epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Alhamisi Mei 30, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581692

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



ZIARA MAKONDA
**WATUMISHI 17** UK. 4
**WASIMAMISHWA MADAI WIZI WA MILIONI 600/-**



# MAGEUZI UJENZI

UKURASA 2, 11 - 16

- Matengenezo barabara, madaraja yaliyoharibiwa na El Nino
- Matokeo chanya kiuchumi sekta kilimo, madini, utalii
- Ujenzi miundombinu kuunganisha SGR, Bwawa la Nyerere
- Ujenzi barabara za mchepuo, mizani, usalama barabarani
- Kuondoa foleni miji mikubwa
- Ujenzi, ukarabati wa vivuko
- Miradi kimkakati viwanja vya ndege
- Barabara za lami kuunganisha mikoa, nchi jirani

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Daktari matatani madai kutoa huduma za rufani kwenye zahanati

UKURASA 2

UKURASA WA 4

**ZIARA YA SAMIA KOREA KUPAISHA ZAIDI TANZANIA HADHI KIMATAIFA**



UKURASA WA 5

**WAPIGAKURA WAPYA MIL. 5.8 KUANDIKISHWA**

UKURASA WA 5

**NCHIMBI AKEMEA CHOKOCHOKO ZA UBAGUZI, UKABILA**






## Sugu kidedea, Msigwa chali

UK.3

**MICHEZO** YANGA YAVUNJA REKODI ZAKE ZILIZOPITA UK.24

**KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akimwapisha Balozi Ami Ramadhani Mpungwe kuwa Mjumbe wa Tume ya Mipango, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. Lengo la tume hii ni kusimamia uchumi, mchakato wa upangaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa. **PICHA: IKULU**

# Mageuzi makubwa Ujenzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Ujenzi imewalisha vipaumbele vinane kwa mwaka wa fedha 2024/25 vilivyojikita kuwekeza katika maeneo muhimu kitaifa, ikiwamo ujenzi wa miundombinu inayorahisisha mawasiliano kufikia miradi ya kitaifa, Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere na Reli ya SGR.

Akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara, Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, alisema dhima ya uwekezaji huo inaangalia katika kumboreshea mwananchi wa kawaida fursa za kiuchumi na kuondoa msongamano katika mji mkubwa.

Makadirio hayo ni zaidi ya Sh. trilioni 1.7 ambazo ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na utekelezaji wa miradi ya maendeleo itakayoleta matokeo chanya ya kiuchumi katika utalii, kilimo, madini, bandari, viwanda na Bwawa la Kufua Umeme la Nyerere.

Alivitaja vipaumbele vingine kuwa ni kufanya matengenezo ya miundombinu ya barabara na madaraja iliyoharibiwa na mvua za El Nino na Kimbunga Hidaya.

"Kipaumbele kingine ni miradi ya kupunguza msongamano katika miji mikubwa kama vile Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Dodoma ni moja ya vipaumbele vyetu," alisema.

Bashungwa alikitaja kipaumbele kingine kuwa ni ujenzi wa barabara zinazounganisha makao makuu ya mikoa na nchi jirani kwa kiwango cha lami pamoja na barabara za ulinzi.

Vilevile, kufanya usanifu wa barabara mpya hasa mijini kwa kuzingatia mahitaji ya watumiaji wote wa barabara wakiwamo wanamichezo, watembea kwa miguu na wanaoendesha vyombo visivyo vya moto.

"Miradi ya kimkakati ikiwamo kukamilisha ujenzi wa viwanja vya ndege vya Msalato, Geita, Kigoma, Tabora, Songwe, Mtwara, Sumbawanga, Shinyanga, Iringa, Musoma, Songea, Tanga na Lake Manyara ni kipaumbele kingine," alisisitiza.

Pia alisema wataendelea na miradi ya usalama barabarani ikiwamo kujenga mizani, barabara za michepuo na njia za waenda kwa miguu na watumiaji wengine wa barabara pamoja na miradi ya ujenzi na ukarabati wa vivuko miradi ya nyumba na majengo ya serikali.

Waziri Bashungwa alisema katika kipindi hicho, wizara itaendelea na matengenezo ya barabara na madaraja kwa kutumia makandarasi wa ndani kwa asilimia 100 na kuhakikisha barabara zinapitika majira yote ya mwaka.

"Pia kuendelea kukijengea uwezo Kitengo cha Ushauri Elekezi wa Miradi cha TANROADS (TANROADS Engineering Consulting Unit - TECU) ili kiendelee kusimamia miradi mikubwa ya kimkakati," alisema.

Alisema wizara pia itafanya mapitio ya Sera ya Ujenzi (2003) na Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani (2009) pamoja na kanuni na miongozo mbalimbali inayohusiana na sekta ya ujenzi, ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia na tabianchi.

Mpango mwingine wa wizara, alisema ni kuendelea kuwajengea uwezo wataalamu wa ndani kupitia programu mbalimbali ili kuongeza wataalamu wabobezi wa ndani kusimamia miradi mikubwa inayoendelea kutekelezwa.

"Kuendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika utendaji kazi, kutumia teknolojia za gharama nafuu katika ujenzi wa barabara hususan katika maeneo korofi na kutekeleza mkakati ya uimarishaji wa utendaji kazi wa TEMESA wa mwaka 2024-2034," alisema.

Kuhusu ushirikishwaji wa sekta binafsi katika miradi ya ujenzi, alisema Tanzania inapoendelea kukua kiuchumi na kijamii, uhitaji wa miundombinu imara na ya kisasa unaongezeka.

Alisema miradi ya ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji ikiwamo barabara na viwanja vya ndege inagharimu fedha nyingi, hivyo kuhitaji uwekezaji mkubwa.

Sambamba na miundombinu ya barabara, madaraja na viwanja vya ndege, Wizara ya Ujenzi inasimamia miradi ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya serikali, vivuko pamoja na karakana za matengenezo ya magari.

"Hata katika maeneo haya, bado utekelezaji upo chini ikilinganishwa na fursa lukuki za uwekezaji zilizopo katika miradi hii," alisema.

Alisema ili kupunguzia serikali gharama kubwa za utekelezaji wa miradi hiyo sambamba na kupunguza muda mrefu unaotumika katika kutekeleza miradi, kuna haja ya kushirikisha sekta binafsi kwa utaratibu wa kushirikiana na sekta binafsi (PPP).

Aidha, alisema kwa kutambua mchango wa sekta binafsi, serikali imefanya maboresho makubwa kwenye Sheria ya PPP kwa lengo la kuvutia uwekezaji wenye tija na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu.

Waziri Bashungwa alisema maboresho muhimu yaliyofanyika katika sheria hiyo ni pamoja na kuruhusu taratibu mbadala za utatuzi wa migogoro, ikiwa ni pamoja na upatanishi na usuluhishi, pamoja na mashauri ya uwekezaji kusikilizwa kwa kutumia mahakama zitakazokubalika baina ya pande zote mbili badala ya mashauri hayo kusikilizwa katika mahakama za ndani.

Kuhusu ushiriki wa wazawa (Local Content) katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya ujenzi alisema sekta hiyo ni miongoni mwa zile zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa.

Alisema kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), wastani wa mchango wa sekta hiyo katika Pato la Taifa katika kipindi cha miaka kumi (2012 -2022) ni asilimia 14.

"Aidha sekta hii imekuwa ikikua kwa wastani wa asilimia 12 kwa mwaka kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita," alisema.

Alisema serikali imekuwa ikitenga fedha nyingi kila mwaka kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na miradi hiyo hutekelezwa na makandarasi kutoka ndani na nje ya nchi.

"Pamoja na kutengewa kiasi kikubwa cha fedha, uchambuzi wa taarifa za usajili wa miradi ya ujenzi kwa miaka kumi, (2013 - 2023) umebaini ushiriki mdogo wa makandarasi wazawa katika miradi hiyo," alisema.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) ambayo ina jukumu la kusajili miradi inayotekelezwa na makandarasi nchini, kati ya jumla ya miradi 36,839, wazawa walitekeleza miradi 35,351 sawa na asilimia 95.9 ya miradi hiyo.

Hata hivyo, alisema miradi iliyotekelezwa na wazawa ni midogo midogo yenye thamani ya Sh. trilioni 23.749, sawa na asilimia 38.5 ya thamani ya miradi yote iliyosajiliwa na kutekelezwa katika kipindi hicho, ambayo ni Sh. trilioni 61.638.

## Daktari matatani madai ya kutoa huduma za rufani katika zahanati

**Vitus Audax,** TABORA

MTUMISHI katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Kitete Tabora, Dk. Festo Jafari, ambaye ni mmiliki wa Zahanati ya Hossiana Mission katika Manispaa ya Tabora, ameingia matatani baada ya kubainika kuwarubuni wagonjwa wanaopewa rufani kwenda hospitali kubwa na kuwapatia huduma katika zahanati yake kinyume na miongozo ya afya.

Kutokana na madai hayo, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paulo Chacha, alifika katika zahanati hiyo juzi na kuliagiza Jeshi la Polisi kuwakamata mkurugenzi mwenza wa zahanati, Sara Elius, Mganga Mfawidhi wa Zahanati na Ezra Masesu kwa tuhuma za kurubuni wagonjwa wanaopewa rufani.

Pia aliagiza mganga mstaafu ambaye jina lake halikutajwa anayedaiwa kuhusika kutoa huduma hizo na mmiliki wa zahanati hiyo, Dk. Jafari ambaye pia mtumishi katika Hospitali ya Kitete.

Chacha alitoa maagizo hayo baada ya zahanati hiyo kubainika kurubuni wagonjwa wanaotakiwa kupata huduma za kibingwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando jijini Mwanza na kuwalaza kwa zaidi ya siku tatu pamoja na kuwafanyia huduma za upasuaji kinyume cha taratibu.

"Kamateni wote mtachambua kwa makini ni nani anayetakiwa kufikishwa mahakamani kujibu mashtaka kati yao. Pia Katibu Tawala wa Mkoa waandikie barua Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) kwa ajili ya kuwachukulia hatua wahudumu wote wa afya watakaobainika kuhusika kwenye tukio hili," alisema Chacha.

Inadaiwa kuwa wagonjwa waliokuwa wakipewa rufani kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tabora ya Kitete, kwenda katika hospitali kubwa ikiwamo Bugando, walikuwa wanarubuniwa na mmiliki wa zahanati hiyo kisha kuwafanyia matibabu kinyemela katika zahanati yake.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Honoratha Rutatinisibwa, alieleza walivyobaini tukio hilo na athari zake kwamba mgonjwa mmoja, kijana wa miaka 24, alikuwa na tatizo la kuvunjika mfupa wa paja, hivyo alitakiwa akapate huduma za kibingwa lakini wakashangaa kukuta amelazwa kwenye zahanati hiyo.

"Alipewa rufani akamwone daktari bingwa wa mifupa Bugando lakini tukashangaa amelazwa hapa wanampa huduma ambayo si stahiki. Kwa hiyo wangeweza kusababisha madhara kwa huyo mgonjwa," Dk. Rutatinisibwa.

Katika hatua nyingine, Chacha aliagiza zahanati hiyo kufungwa kupisha taratibu za kiuchunguzi pamoja na taratibu za kisheria kwa mujibu wa miongozo ya afya.

HABARI KITAIFA

# Sugu kidedea, Peter Msigwa chali

**Elizabeth Kilindi na Elizabeth Zaya**

MBUNGE za zamani wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi, maarufu kama Sugu, ameibuka mshindi katika nafasi ya Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Nyasa.

Katika uchaguzi wa kanda hiyo uliofanyika ukumbi wa Kanisa Katoliki Parokia ya Makambako, ambao ulikuwa na mchuano mkali, Sugu aliibuka kidedea baada ya kupata kura 52 sawa na asilimia 51 dhidi ya Mbunge wa zamani wa Iringa Mjini, Mchungaji Peter Msigwa aliyepata kura 51 (asilimia 49).

Katika nafasi ya makamu mwenyekiti aliyeibuka mshindi ni Mbunge wa zamani wa Tunduma, Frank Mwajakoka, aliyepata 60. Alikuwa akichuana na Ndengese Anosisye aliyepata kura 43 na Joseph Mwasote aliyeambulia kura tatu.

Grace Shio alichaguliwa kuwa Mtunza Hazina baada ya kupata kura 54 akiwabwaga Getrude Lengesele aliyepata kura 51 na Rehema Makobe kura moja.

Akizungumza baada ya matokeo hayo yaliyotangazwa saa 1:30 jioni, Sugu alisema uchaguzi umekwisha, hivyo wavunje makundi na kushikamana kukijenga chama.

Alisema nguvu kubwa sasa ni kuelekeza katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu ujao wa Rais, Wabunge na Madiwani huku akitanabaisha kuwa CHADEMA ni chama kikubwa. Sugu aliahidi kubeba na kuyaendeleza mazuri yote yaliyofanywa na Msigwa.

Msigwa kwa upande wake, alisema amepokea matokeo hayo na kusema uongozi ni kupokezana na kushindwa katika kinyang'anyiro hicho hakutamwondolea hali aliyo nayo.

Awali, uchaguzi huo ambao ulihusisha kanda zingine za Serengeti na Magharibi, ulitawaliwa na sarakasi tangu asubuhi mpaka jioni. Hatua hiyo ilisababisha mchakato mzima ikiwamo upigaji wa kura kusimama kwa zaidi ya saa tano na nafasi nyingine zikifutwa kabisa kuchagua viongozi wake.

Katika Kanda ya Nyasa, ndiko kulikuwa na 'kivumbi' na vitimbwi vingi kuanzia wajumbe walipoanza kuingia asubuhi kwenye mkutano wa uchaguzi, wakati wa uchaguzi na baada.

Pembeni mwa eneo la uchaguzi, makundi ya wanachama yalionekana yakiimba na kufanya michezo ya bashasha.

Kanda ya Nyasa licha ya kuwapo kwa ulinzi mkali, kutokana na mvuto wa Msigwa na Sugu ambao wamejijengea umaarufu ndani na nje ya chama, kulitokea vurugu za hapa na pale japokuwa zilidhibitiwa na uchaguzi kuendelea kama kawaida.

Kambi za wagombea hao, kila moja ilikuwa ikishangilia ikiamini itaibuka na ushindi hata kabla ya matokeo kutangazwa huku zikirushiana maneno na vijembe.

Uchaguzi huo uliimarishwa ulinzi huku kila mtu aliyekuwa akiingia alikaguliwa huku waandishi wa habari wakizuiwa nje ya geti la kanisa hilo.

Baadaye, Katibu wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, Gwamaka Mbughi, alizungumza na waandishi wa habari na kuwaambia kwamba hawatoruhusiwa kurekodi au kushiriki mchakato mzima wa uchaguzi mpaka wakati wa utangazaji wa matokeo.

Pia ilidaiwa kuwa kuna baadhi ya wajumbe wamechelewa kuingia ukumbini kwa kile kinachodaiwa walifungiwa mahali na kunyang'anywa simu hadi muda wa kupiga kura utakapofika.

Aidha, walinzi wa chama hicho walifanikiwa kumdhibiti mtu mmoja ambaye alionyesha viashiria vya kuazisha vurugu.

Uchaguzi wa nafasi ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Mtunza Hazina, ulisimama zaidi ya saa tano kutokana na sintofahamu kwa baadhi ya wajumbe kudaiwa kukosa uhalali wa kushiriki uchaguzi kwa sababu ya maeneo wanayotoka kuwa na rufani za uchaguzi.

Hata hivyo, baada ya majadiliano, walifikia mwafaka kuwa uchaguzi huo uendelee saa 11: 38 jioni tangu uliposimama saa 8:14 mchana.

Baadhi ya wanachama waliokuwa eneo hilo la uchaguzi, waliozungumza na Nipashe, walidai kwamba kwenye uchaguzi wa mabaraza wengi walioshinda ni wale wanaoungwa mkono na Mch. Msigwa na anayeungwa mkono na Sugu aliyeshinda ni mmoja pekee.

Kanda hiyo ya Nyasa inatajwa kutengeneza makundi mawili ambayo baadhi wanadai kwamba endapo yasipokutanishwa na kusuluhishwa huenda yakasababisha msuguano mkubwa.

Katika Kanda ya Magharibi, uchaguzi wa Mwenyekiti Baraza la Vijana CHADEMA (BAVICHA) ulifutwa baada ya wajumbe kushindwa kuafikiana kumpata mwenyekiti wa kusimamia uchaguzi huo.

Mpaka gazeti hili linakwenda mitamboni, uchaguzi wa wenyeviti, makamu wenyeviti na Mtunza hazina kwenye kanda hizo ulikuwa unaendelea.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA**
**WILAYA YA NJOMBE**
**KITUO CHA NJOMBE MJINI**
**MKOA WA NJOMBE**
**Shauri la madai/Ndoa Na...40/2024**
**ELIZABETH MWANZALILA....... Mwombaji /Mdai**
**EXAVERY NDIMBO..........Mjibu maombi /Mdaiwa**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 15 (2) ya Kanuni ya Kanuni ya Madai Mahakama za Mwanzo)**

Kwakuwa mdai /mdaiwa ameleta/Wameleta maddai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za madai **UNAHITAJIKA KUFIKA MAHAKAMA YA MWANZO NJOMBE MJINI KUJIBU DAI LA TSH. 1,292,000/= )**

Kwaiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 30 Mwezi 05 Mwaka 2024 saa 2:30 Asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea

**ANGALIZO:** Kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na kuthibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Mhuri wa Mahakamani hii leo tarehe 23 Mwezi 05 Mwaka 2024




## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



## HABARI KITAIFA

# Watumishi 17 wasimamishwa madai wizi mil. 600/-

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, ameagiza kusimamishwa kazi watumishi 17 wa idara ya afya kwa uchunguzi, akiwamo Mganga Mkuu wa Wilaya ya Arusha (DMO), Dk. Petro Mboya, kwa tuhuma za ubadhirifu wa zaidi ya Sh. milioni 600.

Makonda pia amemtimua kwenye mkutano wake Ofisa Ardhi wa Halmashauri ya Arusha, Shevednaz Mwakyokola, na kuagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwa alimshuhudia akipokea rushwa ya Sh. milioni tano.

Makonda alitoa maagizo hayo juzi katika mkutano wa hadhara eneo la Ngaramtoni baada ya kumtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, Selemani Msumi, kueleza ubadhirifu wa Sh. milioni 600 uliofanywa na watumishi wa idara ya afya.

"Mkurugenzi njoo kwenye halmashauri yako sekta ya idara ya afya kuna ubadhirifu zaidi ya Sh. milioni 600 watu wamekula ziko wapi na hao watu wako wapi," alisema Makonda huku Msumi akikiri kuwapo kwa tuhuma hizo na kwamba suala hilo liko polisi kwa hatua zaidi.

Baada ya maelezo hayo, Makonda alimwita Mkuu wa Polisi Wilaya ya Arumeru, James Msenga, atoe taarifa kuhusu fedha hizo na waliohusika wako wapi.

Msenga alisema Aprili 13, mwaka huu, walikamatwa na kuwaweka ndani lakini uchunguzi ulifanyika wa Sh. milioni 152.1 na baada ya kukaa ndani kwa siku 10 walipatiwa dhamana.

Makonda alihoji kuna Sh. milioni 333 ziko wapi na Msenga alijibu kuwa mhusika wa kwanza ambaye alikuwa mhasibu msaidizi wa kituo, amekimbia mpaka sasa hajaonekana.

Hatua hiyo ilimfanya Makonda kuhoji: "Mhusika wa umma amekimbia kwa Sh. milioni 333 hivi hivi? Kwa hiyo tumeshindwa kumpata hadi sasa? Alikula hizo fedha peke yake?

Hata hivyo, Msenga alisema Jeshi la Polisi linaendelea kumtafuta ili achukuliwe hatua.



Makonda pia aliuliza na kutaka kujua utaratibu wa kiuchunguzi kama watu wanaochunguzwa wanakuwa bado wako katika majukumu yao ndipo Ofisa Utumishi wa Halmashauri ya Arusha, Elizabeth Ngombei, akasema mtumishi anapotuhumiwa jambo la kwanza wanalilifanya ni kumtaka atoe maelezo ndani ya siku saba.

"Haya nataka kujua siku saba zimeisha au hazijaisha. Mjue taarifa zote ninazo hili kabrasha lote lina nyaraka zenu namjua kila mmoja kwa sura zenu ila sitaki uongo," alisema Makonda.

Makonda aliagiza kipaza sauti kiende kwa OCD huku akimuuliza ni lini ameanza kuchunguza na kujibu ni wiki tatu zimeisha.

Mkuu huyo wa mkoa alimgeukia Ngombei na kumhoji: "Kwa hiyo barua imeandikwa ikiwa tayari uchunguzi umeanza? Kwa hiyo nyie mnachunguza tofauti na polisi?"

Kwa mujibu wa Makonda, fedha hizo zinazodaiwa kutafunwa ni mtandao mmoja kutoka sekta ya afya na una vituo 14 kwenye Sh. milioni 152 ni vituo vinane na Sh. milioni 337 vituo sita.

"Unaweza kuona Arusha DC namna inavyonuka rushwa ndiyo maana leo wameamua kunipeleka kwenye miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamaii (TASAF). Hakuna mradi hata mmoja na mapato yao walionipeleka na hakuna mradi hata mmoja wa fedha zilizoletwa na Rais Samia Suluhu Hassan walionipeleka," alisema.

"Wamenichengesha mbali kilometa 60 wananirudisha na kunipeleka kule juu nikaangalie nyumba ya mwalimu ili hapa katikati nisione kinachoendelea, watakula 'spana' mpaka watanyoka. Polisi wana wiki tatu wao hata siku saba hawana. maana yake polisi imeanza uchunguzi mwajiri hujui," alisema.

Aidha, Makonda alisema kuhusu Sh. milioni 600 anaujua mtandao wake ni mkubwa na wako wakubwa ambao wanahusika kutoka wizarani.

"Ili tuwapate lazima tuwakamate hawa na utaratibu huwezi kumchunguza mtu yuko ofisini au mimi ndio sijui utaratibu ofisa utumishi? Tunamchunguza mtu huku akiwa anaendelea na kazi? "alihoji Makonda.

Alisema haiwezekani watu waliowaibia wananchi wakaendelea kujilipa mishahara la sivyo wanawalinda watuhumiwa hao.

"DMO uko wapi? Na wewe upo katika hiyo orodha? kuanzia sasa hivi hawa wasimamishwe kazi. Polisi anzeni kazi yenu vizuri, nataka ndani ya siku saba nipate ripoti," alisema Makonda.

Awali, alipoingia katika mkutano huo, baada ya kuwasalimia wananchi, alisema amemwona Ofisa Ardhi Mwakyokola wakati alishaagiza achunguzwe kwa tuhuma za rushwa.

"Hapa tulipo nimemuona mtumishi ambaye nilishasema sitaki kumwona, ninataka achunguzwe. Lakini nimemuona yupo hapa Ofisa Ardhi njoo hapa. Uko chini ya ulinzi uchunguzi uendelee.

"Nilimkuta kwa macho yangu anachukua Sh. milioni tano ya rushwa. Simama wewe unajua, njoo hapa bwana. TAKUKURU anzeni naye kwa macho yangu, nimemuona alivyo mtu wa ajabu akaitupa ile hela ili asionekane na ushahidi upo. Nimeshasema ni bora siku moja nikae kinywani kwa bwana kuliko siku 1,000 nikae na wadhalimu," alisema.

Makonda alisema siku aliyokuja Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Mwinyi mkoani Arusha, alimuona kwa macho yake anapewa fedha. Alimfuata na kumwambia ampatie hiyo bahasha akaitupa isionekane na ushahidi wa video anao.


AZANIA BANK
Banking Beyond Ordinary

## NOTICE TO SHAREHOLDERS

Notice is hereby given that the 31st Annual General Meeting of the Shareholders of Azania Bank Plc will be held at Kivukoni Hall, Dar es Salaam Serena Hotel, Ohio Street in Dar es Salaam on Saturday 22nd June, 2024 starting from 10.00am with the following agenda:

1. **Opening the Meeting**
   To open the meeting.
2. **Notice and Quorum**
   To read the notice and determine if quorum is present.
3. **Adoption of the Agenda**
   To receive and if appropriate adopt the proposed agenda.
4. **Confirmation of Minutes**
   To confirm minutes of 30th Annual General Meeting held on 29th April, 2023.
5. **Report on Matters Arising**
   To receive a report on the matters arising from the minutes of the 30th Annual General Meeting.
6. **Directors Report**
   To Receive Directors Report through Chairman's Statement.
7. **Financial Statements for the year ended 31st December, 2023**
   To receive and approve the Audited Financial Statement for the year ended 31st December, 2023.
8. **Proposal for Declaration of Dividend from the Profit obtained in 2023**
   To receive and discuss proposal for payment of dividend from the profit obtained in 2023.
9. **Composition of the Board of Directors and Remuneration**
   To take note of the Composition of the Board of Directors and approve Directors Remunerations for the year 2024.
10. **Appointment of External Auditor**
    To appoint the External Auditors for the year 2024.
11. **Any Other Business**

Any shareholder entitled to attend and vote at the meeting is entitled to appoint a proxy to attend and vote on his behalf. The proxy should reach the registered office of the Bank not less than 24 hours before the time of the meeting. Holders of proxies are required to bring with them acknowledgements of receipt of delivery of proxy forms and identification card for registration purposes.

Contact for Communication is;
Company Secretary,
Azania Bank Plc,
Ground Floor, Mawasiliano Towers,
20 Sam Nujoma Road,
P. O. Box 32089,
Dar es Salaam.
Tel +255 22 2412025/6/7
Email: info@azaniabank.co.tz

**By Order of the Board**
Charles Mugila

**Company Secretary**
29th May, 2024


# Ziara ya Rais Samia Korea kupaisha Tanzania kimataifa

**Na Halfani Chusi**

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajia kufanya ziara ya kikazi ya siku sita Jamuhuri ya Korea, ambayo itakuwa na manufaa katika sekta mbalimbali kwa Tanzania.

Katika ziara hiyo, Rais Samia pia anatarajiwa kutunukiwa Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa (Doctorate Honoris Causa) na Chuo Kikuu cha Anga Korea (KAU), kwa kutambua mchango wake katika mabadiliko ya sera na uongozi wa kimantiki.

Hii ni shahada ya tano ya heshima kwa kiongozi huyo baada ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Chuo Kikuu cha Jawaharlal Nehru cha India na hivi karibuni alitunukiwa na Chuo Kikuu cha Ankara, Uturuki, kwa kutambua mchango wake kwenye nyanja mbalimbali.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu manufaa ya ziara hiyo kwa Tanzania, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, alisema ziara hiyo ni ya kikazi kwa mwaliko wa Rais wa Jamuhuri ya Korea, Yoon Suk Yeol.

Alisema ziara hiyo itaanza leo hadi Juni 6, mwaka huu, na kwamba viongozi hao watafanya mazungumzo maalum Ikulu ambayo yatajikita katika uhusiano kati ya nchi hizo mbili.

Pia alisema katika ziara hiyo, Rais Samia atashuhudia utiaji saini mikataba mbalimbali ukiwamo wa mkopo nafuu wa Dola bilioni 2.5 kusaidia miradi ya maendeleo katika elimu, afya na miundombinu kwa miaka mitano.

Mingine ni ushirikiano wa masuala ya anga, uchumi wa buluu, madini ya kimkakati, kilimo, utamaduni na sanaa.

Alisema kutakuwa na hati ya makubaliano kati ya taasisi ya utafiti wa madini nchini na ya sayansi ya miamba nchini humo, utafiti uchoraji ramani za rasilimali, makubaliano ya maendeleo ya uchumi wa buluu, kutambua vyeti vya mabaharia, tamko la pamoja la uanzishaji wa majadiliano juu ya mkataba wa ushirikiano kiuchumi.

Kwa mujibu wa Makamba, Rais Samia atahutubia mkutano kati ya serikali ya Korea na wakuu wa nchi za Afrika, utakaofanyika Juni 4 na 5 kwa lengo la kutoa maoni katika jopo la Kuimarisha Usalama na Chakula na Madini.

Eneo lingine ni Diplomasia ya uchumi na kikao na viongozi wa kampuni kuu za Korea kwa ajili ya kuangalia uwezekano wa kushirikiana katika sekta za nishati, miundombinu na utayarishaji wa filamu.

# Nchimbi akemea chokochoko ubaguzi

**Na Romana Mallya, SINGIDA**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, amesema watu wanaoshabikia mgawanyo wa watu kwa misingi ya ukabila au maeneo ya nchi ama kwa kutokujua au kujua, nia yao ni kulipasua taifa.

Amewataka Watanzania wasikubali kuacha umoja wao kwa kugawanywa na kufarakanishwa, waendelee kuwa wamoja na Tanzania ibaki kuwa na umoja na upendo.

Akizungumza na wananchi wa wilaya ya Manyoni, mkoani Singida jana katika mkutano wa hadhara ikiwa ni siku yake ya kwanza ya ziara yake ya kutembelea mikoa mitano, Balozi Nchimbi alianza kwa kusikiliza kero za wananchi na kuzitolea ufafanuzi.

Balozi Nchimbi alisema: "Katika matangazo mbalimbali ya runinga na redio huwa mnasikia neno linalosema, safari moja huanzisha nyingine. Kila kitu kikubwa sana duniani kilianza na safari ndogo, kila vita kubwa duniani ilianza na jambo dogo.

"Kila ugomvi mkubwa wa watu wanauana ulianza na safari ndogo. Kuna watu mnajua wanakutana wawili hawajawahi hata kuonana umemkanyaga kwa bahati mbaya anakupiga kibao na wewe unajibu mara amekufa.

"Baadaye ukiulizwa hivi ilikuaje yule mtu mpaka akafa, alikanyagwa kidogo au alisukumwa kidogo, kilichotokea ni safari moja huanzisha nyingine.

Katibu Mkuu huyo alisema hivi karibuni baadhi ya watu wameanza kuongelea makabila, mgawanyo wa maeneo ya nchi na wengine wanaongelea Bara na Zanzibar.

"Baadhi ya watu wameanza kuongelea Watanganyika hatunufaiki na muungano, Wazanzibar hatunufaiki na muungano, safari moja huanzisha nyingine. Watu wanaoshabikia mgawanyo wa watu kwa misingi ya makabila au maeneo ya nchi yetu ama kwa kutokujua au kujua wanaelekea kulipasua taifa," alisema.

Nchimbi alisema itatokea Wazanzibari watachochewa na watu wasiokuwa na upeo wakawakataa Watanganyika na Watanzania Bara watachochewa na kuwakataa Watanzania Zanzibar.

"Siku moja tutalala tutaamka Wazanzibar hawawataki kabisa Watanzania Bara. Watanzania Bara hawawataki Wazanzibar, safari moja huanzisha nyingine. Tukimaliza hilo tutaanza safari nyingine watu wa Singida hawawataki watu wa Manyara, watu wa Mbeya hawataki watu wa Songwe, watu wa Tabora hawataki watu wa Mwanza," alisema.

Kutokana na hali hiyo, Balozi Nchimbi aliwaomba Watanzania wakatae mbegu ya kuligawa taifa, na kila anayeongea maneno ya kuligawa taifa kwa misingi ya eneo au ukabila ajue kuwa, Watanzania wanakasirishwa na tabia hiyo.

"Mwonyesheni waziwazi kwamba hamfurahishwi na unachofanya. Waliozaliwa kabla ya 1964 kabla ya uwanja huu wanyooshe mkono, karibu uwanja mzima, halafu kuna mtu mmoja anaibuka hapa anaanza kusema ooh! Turudi Tanganyika.

"Tumeshazoea Tanzania yetu, kataeni watu hao wasiturudishe nyuma, tuseme tunataka kuiboresha nchi yetu. Waasisi wetu hawakutaka tuishie kwenye Tanzania tu, walitaka Afrika Mashariki iwe nchi moja, walitaka Afrika iwe nchi moja. Tumefika tuifanye Afrika Mashariki iwe nchi moja, Afrika tuwe moja tunataka turudi nyuma kuigawanya na hiyo moja tuliyopata?" Alihoji.

"Tusikubali kuacha umoja wetu ninawaombeni sana. Tusikubali kugawanywa, tusikubali kufarakanishwa, Tanzania iendelee kuwa nchi moja yenye mshikamano, yenye upendo, ambayo haibagui watu wake kwa tofauti ya ukabila, dini wala vyama vya siasa. Wote ni Watanzania nchi ni yetu wote, tuishi kwa kushirikiana," alisisitiza.

Akijibu hoja ya mwananchi aliyetaka serikali iunganishe vijana wenye fani mbalimbali na kuwapa mitaji na kuwasaidia kazi zinapokuwapo, Balozi Nchimbi alisema ushauri huo ni mzuri na unaotakiwa kufanyiwa kazi, huku akisisitiza kuwa, vijana wajielekeze kwenye kujiajiri.

"Wanaweza kujiajiri vizuri kama wanatengenezewa mazingira bora. Nitoe wito kwa serikali za mitaa nchi nzima kutambua vijana wasomi wa fani mbalimbali tunapokwenda kuanza kutoa mikopo ambayo imeshapitishwa na Rais Samia Suluhu Hassan, mzingatie makundi ya vijana wasomi na muwape ushauri namna ya kujiunga pamoja na kufanya kazi pamoja.

Akijibu kuhusu kero ya umeme kukatika kutokana na kutokuwapo na 'Substation' (kituo cha kuongeza nguvu umeme), Balozi Nchimbi alisema amempigia simu Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko na kumweleza ombi hilo ambaye amemhakikishia atalifanyia kazi.

Kuhusu malalamiko ya wenye ulemavu yaliyotolewa wilayani hapo kuwa, hawapewi nafasi wanapoomba huku majina yao yamekuwa hayarudi, Balozi Nchimbi alisema ni sera ya CCM walemavu kupata nafasi na kuwataka viongozi kuongeza kasi kwao ili wananchi waridhike.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Taifa, Amos Makalla, alisema Rais Samia anaingia katika rekodi ya kubadilisha hali za wananchi wakiwamo Singida, huduma za kijamii zimeongezeka.

Kadhalika, alisema CCM ina mkakati na wananchi wake ambapo kimejielekeza kuielekeza serikali kutekeleza ilani.

"Tumekuja kuwatembelea kuangalia uhaki wa chama, maandalizi ya uchaguzi, utekelezaji wa ilani na mafanikio, kutatua kero mbalimbali. Leo asubuhi tumepokea taarifa za chama hakika hatuna mashaka tumejiridhisha, uhai wa CCM upo imara Singida.

"Tumejiridhisha maandalizi ya uchaguzi yanakwenda vizuri na msingi wetu tunataka kuujenga katika uchaguzi wa mitaa ili tushinde kwa kishindo ili mwakani tushinde pia kwa kishindo," alifafanua.




Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Kailima Ramadhani akizungumza na waandishi wa habari, mjini Kigoma jana, kuhusu uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura unaotarajiwa kufanyika mkoani humo kwa siku saba kuanzia Julai 01 hadi 07 mwaka huu. **PICHA: TUME**

# Wapigakura wapya milioni 5.8 kuandikishwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAPIGAKURA wapya 5,586,422 wanatarajiwa kuandikishwa nchi nzima, wakati wa uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura unaotarajiwa kufanyika mkoani humo kwa siku saba kuanzia Julai Mosi, mwaka huu.

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Ramadhani Kailima, alisema jana kuwa idadi hiyo ya wapigakura ni sawa na asilimia 18.7 ya wapigakura 29,754,699 walioko kwenye daftari baada ya uboreshaji uliofanyika mwaka 2019/20.

"Katika zoezi hili, inatarajiwa wapigakura 4,369,531 wataboresha taarifa zao na wapigakura 594,494 wataondolewa kwenye daftari kwa kukosa sifa za kuendelea kuwapo kwenye daftari. Hivyo, baada ya uboreshaji, inatarajiwa kuwa daftari litakuwa na jumla ya wapigakura 34,746,638," alisema Kailima.

Kuhusu idadi ya vituo vya kuandikisha wapigakura, Kailima alisema katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura mwaka huu kutakuwa na vituo 40,126 na kati ya hivyo, 39,709 ni vya Tanzania Bara na 417 ni vya Zanzibar.

Katika mkoa wa Kigoma ambako utafanyika uzinduzi wa uboreshaji huo, alisema wapigakura wapya 224,355 wanatarajiwa kuandikishwa, katika uzinduzi ho, mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani Kigoma, Mkurugenzi wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Ramadhani Kailima, alisema wapigakura hao ni ongezeko la asilimia 21.50 ya wapigakura 1,043,281 waliomo kwenye daftari mkoani Kigoma.

"Kwa Mkoa wa Kigoma ambao una halmashauri ya manispaa moja, halmashauri ya mji mmoja na halmashauri za wilaya sita, majimbo ya uchaguzi manane na kata 488, tume inatarajia kuandikisha wapigakura wapya 224,355.

"Hii ni ongezeko la asilimia 21.50 ya wapigakura 1,043,281 waliomo kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura. Kwa hiyo tume inatarajia baada ya uandikishaji, mkoa wa Kigoma utakuwa na wapigakura 1,267,636," alisema Kailima.

Aliongeza kuwa: "Katika zoezi hili, inatarajiwa wapigakura 4,369,531 wataboresha taarifa zao na wapigakura 594,494 wataondolewa kwenye daftari kwa kukosa sifa za kuendelea kuwapo kwenye daftari. Hivyo, baada ya uboreshaji, inatarajiwa kuwa daftari litakuwa na jumla ya wapigakura 34,746,638," alisema Kailima.

Kuhusu idadi ya vituo vya kuandikisha wapigakura, Kailima alisema katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura mwaka huu kutakuwa na vituo 40,126 na kati ya hivyo, 39,709 ni vya Tanzania Bara na 417 ni vya Zanzibar.

"Vituo hivi ni ongezeko la vituo 2,312 ikilinganishwa na vituo 37,814 vilivyotumika kuandikisha wapigakura mwaka 2019/20," alisema.

Kailima alisema Kigoma ina vituo 1,162 ambavyo vitatumika kwenye uboreshaji wa mwaka huu ikiwa ni ongezeko la vituo 69 kutoka 1,093 vilivyotumika kwenye uboreshaji mwaka 2019/20.

Uboreshaji wa daftari utahusisha uandikishaji wa wapigakura wapya ambao ni raia wa Tanzania wenye umri wa miaka 18 na zaidi na watakaotimiza umri huo ifikapo tarehe ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 pamoja na wale ambao hawajapoteza sifa za kuendelea kuwamo kwenye daftari kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi au sheria nyingine yoyote.

Uboreshaji pia utahusu kutoa fursa kwa wapigakura walioandikishwa awali na ambao wamehama kutoka mkoa au wilaya moja kwenda nyingine kuhamisha taarifa zao kutoka kata au jimbo walioandikishwa awali.

Kazi hiyo pia itatoa fursa kwa wapigakura walioandikishwa kurekebisha taarifa zao yakiwamo majina na taarifa zingine, kutoa kadi mpya kwa wapigakura waliopoteza kadi au kadi kuharibika na kuondoa wapiga kura waliopoteza sifa za kuwamo kwenye daftari kutokana na sababu mbalimbali kama vile kuukana uraia wa Tanzania na kifo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bajeti ujenzi kichocheo kwa maendeleo kiuchumi, kijamii

**MIUNDOMBINU** ya usafirishaji na uchukuzi ni kiungo muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi, ongezeko la pato la taifa na kupunguza umaskini. Ushuhuda katika hilo unajionyesha katika maeneo ambayo hayana miundombinu bora kupiga hatua kubwa za kimaendeleo kuliko zile zenye miundombinu hafifu.

Mikoa ya Kaskazini ya Arusha na Kilimanjaro, Kanda ya Kati (Dodoma) na Nyanda za Juu Kusini ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe ina maendeleo makubwa ya kiuchumi kulinganisha na ile iliyochelewa kupata miundombinu hiyo kama vile Katavi, Kigoma, Tabora, Lindi na Mtwara pamoja na Ruvuma kwa Wilaya za Namtumbo na Tunduru.

Uwapo wa barabara za kiwango cha lami, miundombinu ya reli na viwanja vya ndege pamoja usafiri bora wa majini, hurahisisha usafirishaji wa abiria na mizigo yakiwamo mazao ya wakulima kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Kutokana na ukweli huo, serikali imekuwa ikielekeza fedha nyingi katika uendelezaji wa miundombinu ya barabara, madaraja, reli, viwanja vya ndege ili kuhakikisha kasi ya maendeleo inaongezeka. Kila mwaka, mabilioni yamekuwa yakitengwa kupitia Wizara za Ujenzi, Uchukuzi na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa ajili ya uendelezaji wa miundombinu ya barabara na ujenzi wa madaraja na viwanja wa ndege.

Katika mwaka ujao wa fedha wa 2024/25, kwa mfano, serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, iliwasilisha makadirio ya mapato na matumizi kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwamo ujenzi wa miundombinu inayorahisisha mawasiliano kufikia miradi ya kitaifa, Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere na Reli ya SGR. Katika kipindi hicho, Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, alisema katika kutekeleza miradi hiyo, wizara imeomba kuidhinishiwa Sh. trilioni 1.7.

Kwa mujibu wa Bashungwa, fedha hizo zinaelekezwa katika uwekezaji wa miradi ya kimkakati ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya barabara itakayofungua fursa za kiuchumi katika sekta za uzalishaji kama vile kilimo, madini, bandari, viwanda, mifugo na utalii. Sambamba na fursa hizo, fedha hizo zinalenga kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja iliyoharibiwa na mvua za El Nino.

Sambamba na vipaumbele hivyo, aliweka bayana kwamba suala la msongamano wa magari katika majiji makubwa kama vile Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Arusha na Mbeya ambayo imekuwa ikisababisha kuzorota kwa shughuli za kiuchumi na kijamii, imepewa umuhimu wa kipekee. Pia barabara zinazounganisha mikoa na zile za nchi jirani kwa ujenzi wa kiwango cha lami, msukumo umewekwa kuhakikisha zinafungua maeneo hayo kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.


Pamoja na hayo, jambo la kufurahisha ni kwamba viwanja vya ndege hasa vya Msalato (Dodoma), Geita, Kigoma, Tabora, Songwe, Mtwara, Sumbawanga, Shinyanga, Iringa, Musoma, Songea, Tanga na Lake Manyara, vimepewa kipaumbele katika hatua mbalimbali za ujenzi ikiwamo baadhi kukamilishwa. Uwapo wa usafiri wa anga, kama itakavyokuwa reli ya kisasa, ni kichocheo kikubwa kwa maendeleo.

Kwa uhalisia na taswira chanya, ni dhahiri kwamba serikali imejizatiti kuhakikisha inaimarisha miundombinu ya uchukuzi na usafirishaji ili kuwaondolea kero wananchi. Wakulima, kwa mfano, wamekuwa wakilalamikia miundombinu mibovu ya barabara kuwa kikwazo kwa maendeleo yao, hivyo, serikali imesikia na imetenga fungu kubwa katika utekelezaji wa jambo hilo.

Pamoja na ukweli huo, kupanga ni jambo moja na utekelezaji ni jambo lingine, hivyo serikali inapaswa kutafuta fedha zilizoombwa na wizara kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo kwa kasi na ufanisi mkubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# NHC ijihadhari na madalali katika mradi wa jengo lake

**PALE** maeneo ya Kinondoni Morocco, Dar es Salaam, mkono wa kushoto ukitokea Mwenge na kulia kama ukitokea mjini, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) limejenga majengo manne, likiwamo la makazi, eneo kubwa la mita 110,000 za mraba.

Shirika hilo limesema, makazi hayo yana kiwanja cha ndege juu ya jengo, katika mradi iliyouita Morocco Square, ambalo jiwe lake la msingi liliwekwa miaka tisa iliyopita na Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, ujenzi ukitarajiwa kugharimu Sh. bilioni 150.

Mwishoni mwa wiki, shiriki hilo limetangaza kuita wafanyabiashara na watu wote wanaotaka kuwekeza kwenye jengo hilo, wazawa na wageni, wito uliotolewa na Kaimu Meneja Mauzo na Masoko wa NHC, Emmanuel Lyimo, akishuhudia mwekezaji wa kwanza katika mradi huo.

"Mpaka sasa tunajivunia tumempata mwekezaji wa hoteli kwenye jengo hili, vile vile tumeuza karibuni asilimia 75 ya nyumba za makazi, upande wa maduka tumekwishapangisha asilimia 100.

"Ofisi pia tumeuza na kupangisha, zimebaki nafasi chache tu, tunatoa wito kwa Watanzania na wawekezaji wote kutumia fursa hii hii, kuchangamkia sehemu zilizobakia," alisema Lyimo.

Pia, akasema NHC imefungua milango ya miradi ya wawekezaji ya ubia. Kwa hili kwanza, nilipongeze shirika hilo kwa kuendelea kujipambanua kuwa ni moja kati ya mashirika machache yaliyosalia nchini kwenye uwezo mkubwa wa kupambana na mazingira na wakati.

Wakati mashirika mengi ya umma yakiwa yamekufa, hilo bado 'linadunda', ambapo nakumbuka wakati huo lilikuwa likijenga nyumba za kota, zilizoitwa 'nyumba za national', ambazo mpaka sasa zinaonekana kwa uchache maeneo ya Tandika, Temeke, Keko, Magomeni, Kinondoni na Mwananyamala, mpaka sasa imeendelea mpaka kujenga maghorofa.

Kitu ambacho kimenisukuma kuandika hili, ni tabia ya kuwapo baadhi ya watu wenye tabia ya udalali kwenye kuwekeza katika nyumba hizo.

Inatajwa kuwa, kuna watu wanapangisha kwenye nyumba au vyumba kwa mikataba na shirika hilo, lakini baadaye nao wanatafuta watu wengine na kuwapangishwa kwa bei ya juu.

Hili huwezi kulielezea kwa lugha nyingine zaidi au udalali, ambapo mtu ananunua kitu kwa bei husika au elekezi, lakini na yeye anatafuta mteja na anauza kwa bei ya juu zaidi ya hiyo.

Vitendo hivi vimetajwa kuwapo hata katika masoko makubwa, ambapo watu wanakodi vizimba, halafu nao wanatafuta wateja kwa kuwakodisha kwa bei kubwa zaidi ya ile.

Hawa watu wanafanya biashara ndani ya biashara, kwa sababu NHC inaweza kuandikishiana na mtu kwa kiasi fulani cha pesa, na yeye anampangisha mwingine kwa bei ya juu, hivyo anapopata kiasi cha pesa kwa mteja wake, anachofanya ni kuilipa NHC kiasi chao, kinachobaki ni cha kwake.

Hii haileti taswira nzuri, kwani inaonekana kama vile gharama za uwekezaji au upangishaji kwa shirika hilo ni kubwa mno na hauzingatii maisha halisi ya Mtanzania, kumbe kuna watu wanapiga 'cha juu.'

Wito wangu wa NHC, kupitia kwa Kaimu Meneja Mauzo na Masoko huyo na mabosi wengine kuangalia namna ya kudhibiti hali hiyo.

Nadhani wao ni wataalamu zaidi, wanaweza kuangalia namna ya kuhakikisha wanaopanga kwenye mradi huo kwenye maeneo ya biashara, ofisi au makazi, kuhakikisha ndiyo hao hao wanaozitumia na hakuna mpangaji mwingine juu ya mpangaji.

Inawezekana ni kufanya ukaguzi kwa wapangaji wao, au chochote kile ambacho wanaweza kubaini kuna tabia kama hiyo ambayo kwa kiasi kikubwa huwaogopesha Watanzania wengi kukataa kuwekeza kwenye miradi ya majengo ya NHC wakihofia ughali wa kodi wakati kiuhalisia sivyo ilivyo.

HABARI KITAIFA

## Biteko aagiza kuundwa baraza makatibu afya

**Na Allan Isack, ARUSHA**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, ameagiza kuanzishwa na kuundwa kwa Baraza la Makatibu Afya ambalo litashughulikia na kusimama masuala yote yanayohusu makatibu afya, ikiwamo nidhamu na maadili kwa watumishi wa kada hiyo.

Amesema kuundwa kwa baraza hilo, kutasaidia kutoa fursa kwa makatibu hao kushughulikia mambo yao kitaaluma kabla ya kupelekwa kwenye vyombo vingine vya uamuzi.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema hayo jana alipomwakilisha Biteko wakati wa mkutano wa mwaka wa kitaaluma wa Chama cha Makatibu Afya Tanzania, mkoani hapa.

"Kuundwa kwa baraza kutasaidia makatibu afya kwa kuwa nyakati nyingine watumishi hawa wanapokumbwa na changamoto mbalimbali za kitaaluma, wanapelekwa kwenye vyombo vingine vya kutoa uamuzi kabla kuanzia kusikilizwa huko kwao kwanza," alisema.

Biteko pia alitoa onyo kali kwa baadhi ya taasisi za serikali zilizoko chini ya Wizara ya Afya kushindwa kufuata na kutambua muundo wa afya, hivyo kusababisha makatibu hao kutekeleza majukumu yao kwa ugumu.

Katika hatua nyingine, aliwataka watumishi hao kurudisha na kuboresha mifumo ya afya nchini ili kutoa huduma bora na za viwango.

Pia alisema serikali kwa kipindi cha miaka mitatu imejitahidi kuboresha sekta ya afya ikiwamo kununua vifaa na vifaa tiba na dawa katika hospitali, vituo vya afya na zahanati nchini.

Aidha, aliwakumbusha watumishi hao wa afya kuzingatia na kusimamia sheria, kanuni na utaratibu wakati wakitekeleza majukumu yao ya kiutumishi.

Rais wa Chama cha Makatibu wa Afya Tanzania, Juliana Mawala, alisema chama hicho kilianzishwa mwaka 1975 na kada hiyo imeendelea kukua na hadi sasa kuna zaidi ya makatibu afya 1,000.

Alisema makatibu hao wako wanaofanya kazi serikalini, taasisi binafsi, mashirika ya maendeleo na kwenye madhehebu ya dini na pia wako waliojiajiri.

Pia alisema lengo la kuwakutanisha makatibu hao ni kujadiliana kuhusu changamoto zinazowakabili na kuangalia na kutumia fursa zilizoko nchini.

Alitaja majukumu mengine kuwa ni pamoja na usimamizi wa masuala ya fedha na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Alisema tangu kuanzishwa kwa chama hicho, wamepata mafanikio mbalimbali ikiwamo kusajili kwa chama na kuwa chombo rasmi katika mfumo wa serikali, wana katiba na kanuni ambazo zimeshaidhinishwa, kufanya mikutano mikuu na kushirikiana na kada nyingi za afya katika utoaji wa huduma.



Balozi wa Marekani nchini, Michael Battle, akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, wakati wa mdahalo baina ya wafanyabiashara wa Tanzania na Marekani, kuhusu namna ya kuondoa vikwazo vya kibiashara. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Balozi wa Marekani ataka ukuaji biashara

**Na Joseph Mwendapole**

BALOZI wa Marekani nchini, Michael Battle, amesema biashara baina ya nchi yake na Tanzania bado ni ndogo, hivyo kutoa wito wa kufanyika mijadala ya mara kwa mara ya kuhakikisha vikwazo vinaondolewa ili kukuza kiwango cha biashara.

Aliyasema hayo juzi wakati wa mdahalo wa biashara uliowakutanisha wafanyabiashara wa Marekani na Tanzania kwa lengo la kujadiliana kuhusu uchumi wa kidijitali, kufikia masoko, maboresho ya kanuni za udhibiti na mazingira ya kibiashara na ziara na maonyesho ya biashara baina ya nchi hizo.

Balozi Battle alisema wafanyabiashara wa Tanzania na Marekani watajadiliana kuhusu vikwazo vya kibiashara na kwa pamoja na kutoa mapendekezo ya namna ya kuviondoa kama sehemu ya kukuza biashara kwa haraka baina ya mataifa hayo.

Alisema mpango wa AGOA ambao unawawezesha wafanyabiashara wa Tanzania kuuza bidhaa zao kwenye soko la Marekani utahuishwa kwa miaka mingine 16 ili kuendelea kukuza biashara ya Tanzania kuingia kwenye soko la Marekani.

"Midahalo ya kibiashara ni njia muafaka ya kukuza biashara ya Marekani kuja hapa nchini na vilevile itastawisha biashara za Tanzania kuingia Marekani ndiyo sababu tunaona umuhimu wa kuwa na mijadala kama hii mara kwa mara ili tuondoe vikwazo vilivyopo.

"Biashara ambayo tunafanya baina ya mataifa yetu ni ndogo sana na sijaona sababu ya kuendelea kuwa kidogo hivi kwahiyo lazima tuwe na mijadala ya mara kwa mara kuhakikisha tunaondoa vikwazo vyote," alisema.

Alisema kwa kutumia teknokojia ya kidijitali kutaleta mageuzi na ukuaji wa kiuchumi pamoja na kupanuliwa kwa wigo wa uchumi na kwamba kuwezesha mifumo ya kidijitali ya utoaji wa huduma za serikali hadi kuwezesha biashara ndogo ndogo na za kati na kwamba mambo yote hayo yanahitaji miundombinu ya kidijitali.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdalah, alisema takwimu zinaonyesha kuwa biashara kati ya Marekani na Tanzania imeendelea kukua na kufikia Dola za Marekani milioni 476 mwaka 2023 kutoka Dola milioni 309 mwaka 2016.

"Hii inaonyesha kwamba bado tuna fursa kubwa ya kuongeza kiasi cha biashara baina ya mataifa yetu haya kwa miaka ijayo kama tutatumia kwa ufasaha fursa zilizopo, Tunaamini midahalo ya kibiashara baina yetu itasaidia kutufikisha sehemu nzuri," alisema.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**



THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE,
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT AUTHORITY

KINONDONIMUNICIPAL COUNCIL

Ref. No: HB.118/258/01/64 — 30th May, 2024

# VACANCY ANNOUNCEMENT

Kinondoni Municipal Council Football Club (KMC FC) invites dynamic and suitable qualified personnel to fill vacant posts as mentioned below:

**THE KINONDONI MUNICIPAL COUNCIL FOOTBALL CLUB (KMC FC)**

The Kinondoni Municipal Council Football Club (KMC FC) owned by Kinondoni Municipal Council is a registered Limited Company under The Companies Act, 2002. The Club is one amongst the Sports Club that participate in National Premier League. The Club has the following vacant posts: -

**1. CHIEF EXECUTIVE OFFICER- 01 POST**

**1.1 DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. Provide Leadership and direction to the entire Club through approved policies, rules, guidelines and procedures regarding strategic and operational plans and market the Club to the Management team and interpret/disseminate same through meetings, directives, circulars, highlighting pertinent areas of attention or concern aiming at leading them through the right direction for overall positive performance of the Club,
ii. Approve proposals on Operational guidelines after carefully scrutinizing and satisfying oneself the directions in which they address the core business performance areas and solicit for Board's approval prior to implementation with a view to maintain the vision and mission of the club,
iii. Secure adequate sources of financing through appealing budget and from various local and international sources with a view to sustain financial capabilities of the club,
iv. Prepare and submit to the Board quarterly and annual comprehensive action plans, budgets and training needs and performance highlighting areas requiring support from the Board in order to maintain performance standards and ultimate achievement of Club goals,
v. Maintain proper communication and relationship with partner institutions as well as internal and external stakeholders through forums, exhibitions, and media with a view of creating, attracting and maintaining awareness of the Club activities enhancing the club image,
vi. Monitor all operational with a view to observe implementation of activities and obtain suggestions and advice corrective measures aimed at activating, supporting and harmonizing efforts towards achieving desired goals,
vii. Create conducive atmosphere by advocating compliance to rules and regulations that are in line with statutory requirements, such as auditing for financial and systems control; inspections of training centers to meet statutory compliance, with a view to attaining regulative and legislative obligations.

**1.2 QUALIFICATIONS**
Holder of Master's Degree in Business Administration or equivalent qualifications from a recognized university/institution with working experience of at least thirteen (13) years of relevant work experience, five (5) of which must be at a senior management position in a reputable institution. Must have a strong background on strategic management and be computer literate with advance knowledge on planning and investments management packages.

**1.3 REMUNERATION**
Attractive remuneration package

**2. HEAD OF FINANCE AND ADMINISTRATION - 01 POST**
Head of the Finance and Administration is overall in-charge of financial management and Administration matters of the Club;

**2.1 DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. Advises the CEO on all financial and Administration matters of the Club;
ii. Prepare annual plan and budget by reviewing and consolidating plans and budgets from his subordinate for onward submission;
iii. Plan, organize, develop and direct financial policies, systems and procedures through analytical approaches and application of national and international accounting and other standards for the purpose of proper utilization of financial resources;
iv. Develop and direct, investment policies by analyzing the internal and external factors to ensure strategic financial management including short term and long-term investments which are in line with objectives of Cub;
v. Administer all Administration works of the Club.
vi. Oversee all Human Resources activities of the Club
vii. Produce Financial Statements by coordinating and directing preparation of consolidated financial reports for management evaluation of performance review by External Auditors and approved by the Board.
viii. Promptly processing of payments to suppliers of goods and/or services to the Club by analyzing and scrutinizing payment requests to ensure that debts balance is at acceptable level.
ix. Promptly processing of payments to suppliers of goods and/or services to the Club by analyzing and scrutinizing payment requests to ensure that debts balance is at acceptable level;
x. Administer proper use of Club funds, insurance and royalties;
xi. Process timely payments of salaries and emoluments;

**2.2 QUALIFICATIONS**
Holders of Master's Degree in Accountancy, Finance, Commerce or Business Administration majoring in Accountancy or Finance or equivalent qualifications from recognized institution and who possess CPA (T), ACCA, ACA, CIMA and registered by NBAA under "Associate" or "Fellow" category with working experience of at least ten (10) years in similar fields five (5) of which must be at senior administrative position.

**2.3 REMUNERATION**
Attractive remuneration package

**3. HEAD OF LEGAL SERVICE - 01 POST DUTIES AND RESPONSIBILITIES**
i. Provide statutory service for the Board in accordance with the Club charter, by-Laws, Regulations and other legal requirements;
ii. To assist the preparation of Annual Budget for the Board and other statutory Committees of the Club;
iii. Custodian of the Club Seal;
iv. Custodian of legal documents including contracts that the Club has entered with individuals, organizations, institution etc.
v. Authenticate legal correspondences addressed to the Club;
vi. Liaise with external regulators and advisers.
vii. Vet all documents emanating from outside in which the Club has an interest;
viii. Participate in preparation of Board meetings schedule and papers.
ix. Serve as overall in charge of the Legal Services in the Club by providing legal advice to the Club;
x. Liaise with the High Court and courts subordinate there to, various institutions, Government Ministries and Departments on Legal matters;
xi. Assist CEO to respond to legal inquiries about the Club operations.

**3.2 QUALIFICATIONS**
Holders of Master's Degree in Law and Registered Advocate of the High Court of Tanzania with at least twelve (12) years of relevant work experience in legal practice and must be computer literate with a strong background on government systems.

**3.3 REMUNERATION**
Attractive remuneration package.

**4. MARKETING MANAGER - 1 POST**

**4.1 DUTIES AND RESPONSIBILITIES**
i. Manage and coordinate marketing and creative staff
ii. Lead market research efforts to uncover the viability of current and existing products/services.
iii. Collaborate with media organizations and advertising agencies.
iv. Brainstorm ideas for new campaigns.
v. Coordinate with the sales team and other Departments to produce effective strategies
vi. Monitor current campaigns, ensuring their staff meets deadlines and complete necessary tasks.

# Watakaofaulu masomo ya sayansi kusomeshwa bure

**Na Hamida Kamchalla,**

TANGA

SERIKALI imesema wanafunzi 700 watakaofaulu vizuri masomo ya sayansi na wakihitaji kusoma vyuo vya hapa nchini, watasomeshwa bure.

Aidha, wanafunzi watakaosoma masomo ya sayansi, uhandisi, Tehama, elimu tiba na hisabati hawatakuwa na gharama za kulipia, kwamba serikali itawagharamia kila kitu.

Hayo yalisemwa juzi na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda wakati akizindua maadhimisho ya elimu, ujuzi na ubunifu yaliyofanyika kitaifa katika Mkoa wa Tanga.

"Siyo mikopo, serikali itakulipia gharama zote ikiwamo kujikimu, malazi na chakula mpaka umalize kusoma, ili mradi waendelee kufanya vizuri kwenye masomo yao kwenye vyuo wanavyosomea," alisema Prof. Mkenda.

Vilevile alisema kupitia ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), imeelekeza kuendeleza sayansi na teknolojia na Rais Samia Suluhu Hassan aliagiza zitengwe fedha kwa ajili ya kuwasomesha vijana wanaofanya vizuri katika masomo ya sayansi.

Alisema serikali iko katika mchakato wa kujenga shule 100 za mafunzo ya amali kwa nyanja ya ufundi kwa nchi nzima, ili kuwawezesha vijana wa kitanzania kujiajiri au kuajiriwa kupitia ujuzi watakaopata kwenye vyuo hivyo.

Kadhalika, Prof. Mkenda amezindua rasmi mwongozo wa Samia Scholarship, kwenda kusomea elimu ya juu ya nyuklia nje ya nchi, ikiwa ni pamoja na kuongeza madirisha ya wanaotaka kwenda kusomea.

Licha ya kuzungumza hayo, alisema maonesho hayo ni chachu ya maendeleo kwa sekta ya elimu katika ubunifu na kusisitiza kuwa wenye ubunifu wajipange na kuwania fursa iliziko kwenye maadhimisho hayo.

Alisema: "Watu wote wenye ubunifu wajipange na wakae tayari kwa kuwa maonesho haya yatafanyika kila mwaka, pia yatafanyika walau kwa miaka miatatu katika mkoa huu, hivyo usilalamike fursa iko njoo uonyeshe ubunifu wako".

Naye Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alisema ili kuendana na kasi ya maendeleo duniani inapasa kufanya mabadiliko makubwa ya sayansi na tekinolojia.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Husna Sekiboko, alisema Bunge linatamani kuona bunifu zinazoibuliwa zinaboreshwa kwa dhana ya kuleta tija na kutatua kero mbalimbali za kijamii.

# Maofisa ugani waagizwa kutengeneza rejista

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

SERIKALI mkoani Kilimanjaro imeendelea kusisitiza juu ya maofisa ugani, kilimo na mifugo kuhakikisha wanawatembelea wafugaji wakati wote ili kutengeneza rejista za huduma za ugani.

Pia, wametakiwa kuhakikisha wanapowafikia wahusika wanajaza taarifa zao ili kuongeza uwajibikaji kwa watumishi hao.

Kauli hiyo, imetolewa na Katibu Tawala Mkoa wa Kilimanjaro, Tixon Nzunda, wakati wa maadhimisho ya wiki ya maziwa yaliyofanyika katika Kata ya Bomang'ombe Wilaya ya Hai mkoani hapa.

Alisema kumefanyika mapinduzi katika sekta ya mifugo ambapo magonjwa yatokanayo na kupe yamepungua kwa zaidi ya asilimia 12, hivyo kiwango cha uambukizaji wa magonjwa hayo kimepungua.

Hata hivyo, alisema serikali imejikita zaidi katika kuongeza thamani ya mazao ya mifugo pamoja na kuhakikisha walaji wanapata usalama wa mazao kutokana na kutengeneza miundombinu rafiki yakuwezesha maziwa kupatikana kwa urahisi.

Alisema kwa mwaka 2023/2024 mkoa huo umepokea dawa za kuogesha mifugo kiasi cha lita 736 ambapo Halmashauri ya Hai ni moja ya wanufaika.

Vilevile alisema serikali imetoa Sh.milioni 100 kujenga kituo cha kukusanyia maziwa Masama ambacho lita 1,500 zilikusanywa katika kituo hicho na wafugaji wapatao 300 walinufaika.

Alisema pia mradi huo na vifaa vinatarajiwa kuwekwa ndani ya mwaka huu wa fedha ili kituo kiweze kuanza kazi mara moja.

Aidha, alisema serikali imetenga bajeti ya Sh.milioni 81.6 kwa ajili ya uanzishwaji wa mashamba darasa ya malisho na mashamba hayo yanatumika kama maeneo ya kufundishia wafugaji namna bora ya upandaji wa malisho ili kuondokana na ufugaji wa kuhama.

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Amiri Mkalipa, aliiomba serikali kuwapatia mitambo kwa wafugaji ili kuongeza uzalishaji, huku akiwataka wafugaji kujitokeza kwa wingi ili kupata elimu ya ufugaji wa kisasa.

Akitoa taarifa ya utekelezaji, Mkuu wa Divisioni ya Kilimo na Mifugo, David Lekei, alisema wilaya hiyo ni miongo mwa wilaya zenye mifugo mingi kwa kuwa ng'ombe wa maziwa ni zaidi ya 49,000 ambao wanafugwa ndani katika ukanda wa kati na mlimani na ng'ombe wa asili wapo zaidi ya 61,000 wanaofugwa kwa wingi maeneo ya tambarare.


vii. Analyze data to evaluate the success of their marketing efforts and come up with new ideas to improve brand marketing and exposure.

**4.2 QUALIFICATIONS**

Holders of a Bachelor's Degree in Marketing, Advertising, Communication or equivalent qualifications form a recognized Institution with at least Ten (10) years of relevant work experience and must be computer literate with a strong background on government systems.

**4.3. REMUNERATION**

Attractive remuneration package.

**5. ACCOUNTANT II - 02 POSTS**

**5.1 DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. To prepare Financial Reports.
ii. To prepare bank reconciliation;
iii. To record and processes financial transactions.
iv. To maintain and update the Fixed Assets Register, and
v. To perform such other related duties as may be assigned by the Supervisor.

**5.2 QUALIFICATIONS**

Holders of Bachelor's Degree in one of the following fields: Accountancy, Finance, Commerce or Business Administration majoring in Accountancy or Finance or equivalent qualification from recognized Institutions and who possess CPA (T), ACCA, ACA, or any professional qualifications recognized by NBAA and registered as an Accountant.

**5.3 REMUNERATION**

Attractive remuneration package.

**GENERAL CONDITIONS:**

i. All applicants must be Citizens of Tanzania with an age not above 45 years of age;
ii. Applicants must attach an up-to-date Curriculum Vitae (CV) having reliable contacts, postal address/post code, e-mail and telephone numbers;
iii. Applicants should apply on the strength of the information given in this advertisement;
iv. Applicants must attach their certified copies of the following certificates;
    - Masters/Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificates;
    - Masters/Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma transcripts;
    - Form IV and Form VI National Examination Certificates;
    - Professional Registration and Training Certificates from respective Registration or Regulatory Bodies, (where applicable);
    - Registration or Regulatory Bodies, (where applicable);
    - Birth certificate
v. Attaching copies of the following certificates is strictly not accepted: -
    - Form IV and form VI results slips;
    - Testimonials and all Partial transcripts;
vi. An applicant should indicate three reputable referees with their reliable contacts;
vii. Certificates from foreign examination bodies for ordinary or Advanced level education should be verified by The National Examination Council of Tanzania (NECTA).
viii. Professional certificates from foreign Universities and other training institutions should be verified by The Tanzania Commission for Universities {TCU) and National Council for Technical Education (NACTE);
ix. An applicant with special needs/case (disability) is supposed/ advised to indicate;
x. A signed application letter should be written either in Swahili or English and

Addressed to:

Municipal Director,
Kinondoni Municipal Council,
P. O. Box 31902,
**DAR ES SALAAM.**

xi. Deadline for the application is **14th day of June, 2024.**
xii. Only shortlisted candidates will be informed on a date for interview

**Released by:**



**Hanifa S. Hamza**
**MUNICIPAL DIRECTOR KINONDONI MUNICIPAL COUNCIL**





# Meli iliyozama Ziwa Victoria yaendelea kusalia majini

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MELI ya Mv. Clarias iliyopinduka na kuanguka majini katika Bandari ya Mwanza Kaskazini, Mei 19 mwaka huu imeendelea kusalia majini, licha ya hivi karibuni kuletwa wataalamu kwa ajili ya kuinyanyua.

Ni zaidi ya siku 10 zimepita tangu meli hiyo iliyokuwa ikifanya safari zake kati ya Kirumba jijini Mwanza na Kisiwa cha Goziba wilayani Muleba mkoani Kagera kuzama katika Ziwa Victoria ambapo mpaka sasa chanzo chake hakijafahamika.

Baadhi ya wadau wa usafiri majini akiwamo, Kitano Chacha, wameiomba serikali kuharakisha mchakato wa kuinyanyua meli hiyo kutoka majini, ili iendelee na shughuli zake, huku wakitaka wafanyakazi wa chombo hicho kunyang'anywa leseni na vyeti ili iwe fundisho kwa wengine na kuacha kufanya uzembe katika vyombo vya umma.

**Tayari tumepata taarifa ya awali lakini taarifa kamili tutaipata pale chombo hiki kitakapotolewa majini na kuwekwa kwenye chelezo.**

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Uwakala wa Meli nchini (TASAC), Mohamed Salum, uchunguzi wa tukio hilo unaendelea na kuwa endapo ikibainika kufanyika kwa uzembe wahusika watachukuliwa hatua kali za kisheria.

"Tayari tumepata taarifa ya awali lakini taarifa kamili tutaipata pale chombo hiki kitakapotolewa majini na kuwekwa kwenye chelezo na iwapo mabaharia watabainika kufanya uzembe tutawachukulia hatua ili kuongeza umakini kwenye matumizi na ulinzi wa vifaa hivi vya umma,"alisema Salum.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Huduma za Meli nchini (MSCL), Erick Hamis, akizungumza kuhusu usalama wa meli katika ukanda wa maziwa makuu alishauri kuwapo kwa kamati ya muda mrefu itakayokuwa ikifanya tathmini mara kwa mara.

Pia alishauri kufanyika kwa utafiti juu ya miamba iliyopo ndani ya Ziwa Victoria na athari zake kwa vyombo hivyo vya usafiri majini.



Mwenyekiti wa Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu J.K. Nyerere, Wilaya ya Serengeti, mkoani Mara, Mtigandi James, akikata utepe kuzindua klabu ya taasisi hiyo ya wanafunzi wa Sekondari Kambarage, mjini Mugumu juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kiongozi wa kata, kijiji jela miaka 3 kwa kuomba rushwa

**Na Halima Ikunji,** KALIUA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora, imewahukumu kwenda jela miaka mitatu Mtendaji wa Kata pamoja na Mtendaji wa Kijiji baada ya kubainika kuomba rushwa ya Sh.milioni tatu kutoka kwa mwananchi aliyekuwa akihusishwa na tuhuma za wizi wa kutumia silaha.

Waliotiwa hatiani katika jinai Na.71/2023 ni Mtendaji wa Kijiji cha Imagi Kata ya Nh'wande, Richard Mpagama na Mtendaji wa Kata ya Nh'wande wilayani hapa, Laurent Sendu ambao kwa pamoja wanaelezwa kutenda kosa hilo Aprili 21 mwaka jana.

Awali waendesha mashtaka wa serikali, David Bakari pamoja na Kajivo Aidan waliiambia mahakama hiyo kuwa viongozi hao waliomba rushwa kutoka kwa Ndilana Budeba ili wamwachie huru.

Alisema Budeba alikuwa akituhumiwa katika kosa lililokuwa likimuhusu mume wa binti yake la kujihusisha na wizi wa kutumia silaha.

Bakari aliiambia mahakama hiyo kuwa kosa hilo ni kinyume cha Sheria ya Mienendo ya Rushwa, Kifungu Kidogo cha 15(1)(a)na (2) cha PCCA, Sura ya 329 Marejeo ya Mwaka 2022.

Akitoa hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Mwandamizi, Felix Ginene, alisema hukumu hiyo ya kwenda jela miaka mitatu au kulipa faini ya Sh.milioni moja kwa kila mmoja iwe fundisho kwa watu wengine wenye nia ovu hasa viongozi wanaoendekeza rushwa ili kutoa huduma kwa wananchi.

Aidha, aliwaamuru wawili hao kumrejeshea Ndilana Budeba Sh. milioni 2.3 ikiwa ni sehemu ya fedha iliyobaki ya kumrejeshea Sh.700,000 wakati uchunguzi wa kesi ulipokuwa unaendelea.

Licha ya watiwa hatiani hao kutakiwa kulipa faini ya Sh.milioni moja kwa kila mmoja ikiwa ni mbadala wa kifungo cha miaka mitatu walishindwa kulipa faini na hivyo wamepelekwa gerezani kutumikia kifungo hicho.

## Wataka unafuu bei pembejeo

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Buchosa wilayani Sengerema wameiomba serikali kusimamia uuzwaji wa pembejeo ikiwamo mbegu za mazao.

Wamesema lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha wananchi wanapata mbegu hizo na kulima kisasa ili kupata mavuno mengi tofauti na sasa.

Madiwani hao akiwamo Diwani wa Kata ya Bungolo, Musa Ngazila, wakati wa maswali katika kikao hicho aliomba kama kuna uwezekano mbegu hizo ziwekewe ruzuku kama ilivyo kwa mbolea, kwamba gharama zake zipo juu zaidi ya mavuno yanayopatikana.

Alisema hatua hiyo itawasaidia wakulima wa chini kutumia mbegu za kisasa kuliko wanavyolima na mbegu za kawaida hali inayosababisha kupata mavuno kidogo na kushusha mapato ya mkulima na halmashauri.

Diwani wa Kata ya Bupandwa, Masumbuko Bupamba, alisema uchumi wa Buchosa unategemea kilimo, hivyo suala la gharama za mbegu kuwa juu na mazao kuuzwa kwa bei ndogo linarudisha nyuma juhudi za wakulima pamoja na shughuli hizo za kiuchumi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Benson Mihayo, alisema serikali imekuwa ikifanyia kazi suala hilo ikiwa ni pamoja na kuweka ruzuku kwenye mbolea na kuhusu gharama za mbegu atalifikisha sehemu husika ili kilimo kwa wananchi wa Buchosa kiendelee kukua.

## Mil.92/- yarejesha miundombinu ya barabara wilayani Maswa

**Na Alex Sayi,** MASWA

SERIKALI imetumia Sh.milioni 92.6 kati ya Sh.milioni 430.5 zilizotengwa katika mkataba Na.S10/022/2023/ 2024/W/43 wa kutekeleza ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara za mitaa (km8) kwa wakazi wa Malampaka wilayani Maswa mkoani Simiyu.

Meneja wa Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Maswa, Justin Lukaga, aliyasema hayo wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa, Dk. Yahaya Nawanda ya kukagua miradi ya maendeleo.

Lukaga alisema matengenezo ya barabara hizo yametekelezwa kama sehemu ya miradi inayotekelezwa na Mkandarasi M/s Njota Investment Co.Ltd.

Alisema mradi huo unajumuisha pia utekelezaji wa Barabara ya Zawa-Mwang'honoli, Malampaka-Mwang'honoli na ujenzi wa madaraja mawili katika Barabara ya Malampaka-Mwang'honoli ambayo kwa pamoja inagharimu zaidi ya Sh.milioni 430.5.

"Mradi wa Malampaka pekee unagharimu Sh.milioni 92.6 kutoka katika mkataba wa miradi hiyo ambapo fedha zake zimetoka katika mfuko wa jimbo ambapo utekelezaji wake ulianza Septemba 25, mwaka jana na umekamilika kwa asilimia 100," alisema Lukaga.

Diwani wa Kata hiyo, Revocatus Mashara, aliishukuru serikali



kupitia wakala huo kwa kufanikisha utekelezaji wa mradi ambapo alidai kuwa ulikuwa umekwama kwa muda mrefu.

"Tunashukuru kwa maana sasa mji wa Malampaka umependeza na barabara za mitaa zinapitika ingawa bado tunamuomba Meneja wa TARURA atuongezee barabara nyingine zaidi ya hizi kilometa nane kwa kuwa bado kunauhitaji mkubwa wa barabara mjini hapa," alisema Mashara.

Mkazi wa Malampaka, Masanja Jidai, alisema matengenezo na maboresho ya barabara katika mji huo yamerahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji na kufanya shughuli zinafanyika kwa urahisi na haraka.





**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI**

# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI MHESHIMIWA INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25 TAREHE 29 MEI, 2024



**Mhe. Innocent L. Bashungwa (Mb.)**
*Waziri wa Ujenzi*



**Mhe. Mha. Godfrey M. Kasekenya (Mb.)**
*Naibu Waziri wa Ujenzi*



**Balozi, Mha. Aisha S. Amour**
*Katibu Mkuu, Wizara ya Ujenzi*



**Bw. Ludovick J. Nduhiye**
*Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Ujenzi*

# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI MHESHIMIWA INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

**A. UTANGULIZI**

1. Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba, kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, iliyochambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi ya mwaka wa fedha 2023/24, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, kwa mwaka wa fedha 2023/24. Ninaliomba Bunge lako Tukufu liridhie kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ujenzi, kwa mwaka wa fedha 2024/25.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama leo hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba Hotuba yangu yote iingie katika kumbukumbu za Bunge kama ilivyowekwa mezani.

3. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako kuwasilisha Hotuba nikiwa Waziri wa Ujenzi, nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Ujenzi tangu tarehe 30 Agosti, 2023. Ninamuahidi Mheshimiwa Rais kuwa kupitia dhamana hii aliyonipa, nitafanya kazi kwa weledi, bidii, uaminifu na ubunifu kwa kushirikiana na watumishi wenzangu katika Wizara na wadau wa Sekta ya Ujenzi, ili kuhakikisha kuwa sekta hii inakua na kuendelea kuwa kichocheo cha maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Kapteni wa jahazi makini, jasiri, mtulivu, mchamungu, mnyenyekevu Chifu Hangaya; ambaye ameongoza nchi yetu kupita mawimbi makali na magumu. Pale Nchi yetu ilipoondokewa na mpendwa wetu hayati Dkt. John Pombe Magufuli (RIP), Rais Samia alituvusha salama katika kipindi hicho cha majonzi na kigumu, alituvusha katika kipindi cha COVID na milipuko ya magonjwa duniani; ametuvusha salama hata kwenye mvua za El Nino na kimbunga Hidaya kwa fedha za dharura, na ameendelea kuiheshimisha nchi yetu katika nyanja za kimataifa na kidiplomasia. Hongera sana Chifu Hangaya, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

4. Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu, na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwa namna ambavyo wanamsaidia Mheshimiwa Rais katika majukumu ya kuitumikia nchi yetu. Nawashukuru pia viongozi hawa kwa miongozo na maelekezo mbalimbali wanayonipatia katika kuisimamia Wizara ya Ujenzi. Ninawashukuru pia Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri wote kwa ushirikiano wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

5. Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, chini ya uongozi wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Selemani Kakoso (Mb. Mpanda Vijijini) na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Anne Kilango Malecela (Mb. Same Mashariki), kwa maelekezo na ushauri wa Kamati ambao umekuwa chachu katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Naishukuru pia Kamati kwa kuchambua kwa kina Taarifa ya Utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2023/24, na kupitisha Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/25. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri, maelekezo na maoni yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika bajeti hii.

6. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu yangu umekuwa rahisi kutokana na ushirikiano mkubwa ninaoupata kutoka kwa viongozi wenzangu katika Wizara. Nawashukuru sana Mheshimiwa Mhandisi Godfrey M. Kasekenya, Naibu Waziri; Balozi Mhandisi Aisha S. Amour, Katibu Mkuu, pamoja na Ndugu Ludovick J. Nduhiye, Naibu Katibu Mkuu. Nawashukuru pia Wakuu wa Idara na Taasisi, Mameneja wa Mikoa wa TANROADS, pamoja na Watumishi wa Wizara na Taasisi zake kwa kujituma katika utekelezaji wa majukumu tuliyokasimiwa Wizarani. Tunamuahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania wote hatutawaangusha.

7. Mheshimiwa Spika, Mhe. Mhandisi Godfrey Kasekenya ni Naibu Waziri mnyenyekevu na mchapa kazi. Ninamshukuru Mhe. Rais kwa kuendelea kumuamini, na tunaahidi kudumisha umoja na mshikamano wa Wizara ili kuendelea kutekeleza Ilani ya CCM kwa spidi na viwango. Ninawapongeza wananchi wa Jimbo la Ileje kwa kuchagua Mbunge makini na mchapakazi. Ninawasihi sana wananchi wa Jimbo la Ileje wampe tena nafasi Bungeni mwakani, kwa mitano tena Mheshimiwa Mhandisi Kasekenya ili kazi iendelee.

8. Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi, kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Rais wa Muungano wa Mabunge Duniani. Imani hii uliyooneshwa kimataifa inaakisi uwezo mkubwa ulionao katika uongozi wa Bunge letu Tukufu pamoja na masuala ya kimataifa.Umeweza majukumu haya mazito yenye kuleta heshima kubwa kwa nchi yetu. Nawaomba wananchi wa Jimbo la Mbeya Mjini waendelee kuwa watulivu na wakupe mitano tena mwakani, kwani wamepata bahati ya kukupata wewe kiongozi hodari na adimu kwa Mbeya. Hongera sana Mheshimiwa Spika. Nampongeza pia Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika, kwa kuendelea kutekeleza vyema wajibu wake katika kukusaidia kusimamia na kuliongoza Bunge letu. Nawapongeza Mwenyekiti wa Bunge Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, pamoja na Wenyeviti wapya wa Bunge waliochaguliwa hivi karibuni Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika. Hongereni sana Waheshimiwa Wenyeviti.

9. Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Karagwe, kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kuwatumikia, pamoja na kutekeleza jukumu la kuwawakilisha humu Bungeni. Ninawaahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu na maarifa yangu yote, ili kuhakikisha Wilaya yetu ya Karagwe inapata maendeleo tunayoyopenda. Asanteni sana Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Karagwe mkiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Cde. Rwamugata, kwa kuwa humu Bungeni leo kuwawakilisha wana Karagwe wenzetu kwenye Bajeti ya Wizara ya Ujenzi.

10. Mheshimiwa Spika, namshukuru pia mke wangu mpendwa Jennifer, (A.K.A Mama Alaska) pamoja na watoto wangu Santo, Solana, Sankara na Samora; kwa namna wanavyonitia moyo, na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu, ili niweze kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi.

11. Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wa Chama cha Madereva wa Serikali leo tunaye humu Bungeni. Kwa nafasi yangu ya mlezi wa madereva wote wa Serikali nchini, nitumie fursa hii kuwapongeza madereva wa Serikali kwa majukumu yao katika kuendesha na kutunza vyombo vya moto vya Serikali. Nitoe wito kwa madereva hawa kuendelea kuzingatia maadili ya utumishi wa umma. Ninawataka wale wachache wanaoharibu taswira nzuri ya madereva wa Serikali, kwa vitendo vilivyo kinyume na maadili, waache mara moja.

12. Mheshimiwa Spika, napenda pia nichukue fursa hii kuwangeza Vijana wa Jangwani (Young Africans) kwa kuvishwa Taji la Ubingwa wa Ligi Kuu ya Tanzania Bara. Niwapongeze pia kwa kuchukua ubingwa mara 3 mfululizo na kuweka historia ya kuchukua ubingwa mara 30 tangu kuanzishwa kwa ligi. Imekuwa timu ya pekee hapa nchini kuweka historia hii.

**B. MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA 6**

13. Mheshimiwa Spika, mwezi Machi 2024, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, alitimiza miaka 3 madarakani. Katika kipindi hicho cha uongozi wake mafanikio makubwa yamepatikana.

**Ujenzi wa Barabara**

14. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani Machi 2021, mtandao wa barabara za lami ulikuwa kilometa 10,830.2. Hadi kufikia Machi 2024, mtandao wa barabara za lami umeongezeka na kufikia kilometa 12,028.7. Katika kipindi cha miaka 3 ya Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa madarakani, miradi ya barabara 25 zenye jumla ya kilometa 1,198.5 imekamilika kujengwa katika mikoa mbalimbali nchini. Barabara hizo ni:

i. Ujenzi wa barabara ya Tabora (Usesula) – Koga – Mpanda; (Lot 2): Komanga – Kasinde (km 120) mkoani Tabora;
ii. Ujenzi wa barabara ya Tabora (Usesula) – Koga – Mpanda; (Lot 3): Kasinde – Mpanda (km 118) mkoani Katavi;
iii. Ujenzi wa barabara ya Tabora (Usesula) – Koga – Mpanda (Lot 1): Usesula – Komanga (km 115) mkoani Tabora;
iv. Ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai –

**Kasanga Port (km 107) mkoani Rukwa;**

v. Ujenzi wa barabara ya Nyahua – Chaya (km 85.4) mkoani Tabora;
vi. Ujenzi wa barabara ya Mbinga – Mbamba Bay (km 66) mkoani Ruvuma.
vii. Ujenzi wa barabara ya Kidahwe – Kasulu (km 63)mkoani Kigoma;
viii. Ujenzi wa barabara ya Nyamuswa – Bunda – Bulamba(km 55) mkoani Mara;
ix. Ujenzi wa barabara ya Njombe – Moronga (km 53.9)mkoani Njombe;
x. Ujenzi wa barabara ya Moronga – Makete (km 53.5)mkoani Njombe;
xi. Ujenzi wa barabara ya Mpemba – Isongole (km 51.2) mkoani Songwe;
xii. Ujenzi wa barabara ya Makutano – Natta – Mugumu(sehemu ya Makutano – Sanzate (km 50) mkoani Mara;
xiii. Ujenzi wa barabara ya Lusitu – Mawengi (km 50)mkoani Njombe;
xiv. Ujenzi wa barabara ya Nyakanazi – Kakonko (Kabingo- km 50) mkoani Kigoma;
xv. Ujenzi wa barabara ya Loliondo – Mto wa Mbu (sehemu ya Waso – Sale Jct) (km 50) mkoani Arusha;
xvi. Ujenzi wa barabara ya Chunya– Makongolosi (km 39) mkoani Mbeya;
xvii. Ujenzi wa barabara ya Rudewa – Kilosa M(km 24)mkoani Morogoro;
xviii. Upanuzi wa barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) pamoja na madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji mkoani Dar es Salaam;
xix. Ujenzi wa barabara, sehemu ya Kusenyi – Suguti (km 5) mkoani Mara;
xx. Ujenzi wa barabara ya Ardhi – Makongo – Goba (Sehemu ya Ardhi – Makongo -km 5) mkoani Dar es Salaam;
xxi. Upanuzi wa barabara ya Morocco – Mwenge (km 4.3) mkoani Dar es Salaam;
xxii. Ujenzi wa barabara ya Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi/Morogoro Road (Mbezi Mwisho); sehemu ya Wazo Hill – Madale (km 4.2) mkoani Dar es Salaam;
xxiii. Ujenzi wa barabara ya Tungi – Kibada (km 3.8) mkoani Dar es Salaam;
xxiv. Ujenzi wa barabara ya Banana - Kitunda - Kivule - Msongola, sehemu ya Kitunda – Kivule (km 3.2) mkoani Dar es Salaam; na
xxv. Upanuzi wa daraja la Gerezani na barabara ya maingilio (km 1.3) mkoani Dar es Salaam.

Katika kipindi hicho cha miaka 3 tangu Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameingia madarakani, jumla ya miradi ya barabara 74 zenye urefu wa kilometa 3,794.1 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kati ya miradi ya barabara hizo 74, utekelezaji wa miradi 12 umefikia asilimia 70 au zaidi, na miradi 62 utekelezaji wake upo chini ya asilimia 70. Miradi hiyo imeoneshwa katika Aya ya 17 ya kitabu cha Hotuba ya Bajeti ya Wizara.

**Ujenzi wa Madaraja Makubwa**

15. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka 3 ya Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa madarakani, madaraja makubwa 8 yamekamilika kujengwa. Madaraja hayo ni:

i. Daraja la Wami mkoani Pwani;
ii. Daraja la Tanzanite mkoani Dar es Salaam; iii. Daraja la Gerezani mkoani Dar es Salaam; iv. Daraja la Mpwapwa mkoani Dodoma;
v. Daraja la Kiyegeya mkoani Morogoro;
vi. Daraja la Ruhuhu mkoani Ruvuma;
vii. Daraja la Kitengule mkoani Kagera; na
viii. Daraja la Msingi mkoani Singida.

Katika kipindi hicho, ujenzi wa madaraja makubwa 5 upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:

i. Daraja la J.P. Magufuli (Kigongo – Busisi) mkoani Mwanza, 88% na tunalenga likamilike kufikia mwaka huu Disemba 2024;
ii. Daraja la Mbangala mkoani Mtwara, 66%;
iii. Daraja la Pangani mkoani Tanga, 23%;
iv. Daraja la Mbambe mkoani Pwani, 25%; na v. Daraja la Simiyu mkoani Mwanza, 15%.

**Miradi ya Viwanja vya Ndege**

16. Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya 6 imekamilisha ujenzi wa viwanja vya ndege 3 katika kipindi cha miaka 3 ya Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa madarakani, ambavyo ni viwanja vya ndege vya Songea, Mtwara na Songwe. Katika kipindi hicho, Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi ya viwanja vya ndege 7 ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Viwanja hivyo ni: Msalato Airport (56.9% kwa kazi za ujenzi wa miundombinu ya kutua na kurukia ndege) na (22.56% kwa kazi za ujenzi wa jengo la abiria na majengo mengine); Musoma Airport (55%); Iringa Airport (90%); Kigoma Airport (Awamu ya III, 3.7%); Sumbawanga Airport (8.4%); Shinyanga Airport (11%); na Tabora Airport (Awamu ya III, 38%).

Taratibu za manunuzi zinaendelea kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Lake Manyara, Iringa (Awamu ya II) na kiwanja cha ndege cha Tanga.

**Miradi ya Vivuko (TEMESA)**

17. Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya 6 imepata mafanikio makubwa katika utoaji wa huduma za vivuko kupitia TEMESA. Katika kipindi cha kuanzia Machi 2021 hadi Mei 2024 Wizara imeendelea na ujenzi wa vivuko vipya 8 ambavyo vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Vivuko hivyo vikikamilika vitatoa huduma katika maeneo ya Bwiro – Bukondo (Ukerewe), Kisorya (Bunda) – Rugezi (Ukerewe), Ijinga – Kahangala (Magu), Nyakaliro – Kome (Sengerema), Buyagu (Sengerema) – Mbalika (Misungwi), Mafia – Nyamisati (Rufiji) na Magogoni (Ilala) – Kigamboni (Kigamboni). Serikali itahakikisha mkandarasi M/S Songoro Marine analipwa fedha zote ili akamilishe ujenzi wa vivuko hivi ndani ya mwaka huu. Kwa mwezi Mei pekee, mkandarasi huyo amelipwa jumla ya Shilingi bilioni 1.526.

**Miradi ya Nyumba na Majengo ya Serikali (TBA)**

18. Mheshimiwa Spika, mafanikio makubwa yamepatikana katika kipindi cha miaka 3 ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika ujenzi wa nyumba na majengo kupitia TBA. Sheria iliyoanzisha TBA imehuishwa ili kuruhusu TBA kushirikiana na sekta binafsi. Uhuishwaji huu umeleta mabadiliko kwenye majukumu ya TBA ikiwemo kuweza kuuza nyumba kwa watu binafsi. Hali hii itaiwezesha TBA kushirikiana na Sekta Binafsi katika kuendeleza milki nchini na kutafuta vyanzo vya fedha kama mikopo kwani miradi yote ambayo itaendelezwa kibiashara itaweza kupangishwa au kuuzwa kwa watu wote kulingana na hali ya soko. Hii itasaidia TBA kujiendesha na kupunguza utegemezi wa ruzuku.

19. Mheshimiwa Spika, kupitia uhuishwaji huu, TBA inatarajia kujenga jumla ya nyumba 1,056 katika maeneo 5 Jijini Dar es Salaam. TBA pia imeandaa orodha ya maeneo yaliyoiva kwa uwekezaji katika mikoa ya Dodoma (12), Arusha (3), Mwanza (2), Shinyanga (1), Singida (1) na Geita (1) na kuyatangaza kwa umma kwa ajili ya miradi ya ubia. Vilevile, TBA imeanza kushirikiana na Taasisi za kifedha katika kutafuta mikopo ya miradi yake mbalimbali ya kibiashara ikiwemo Canadian (Masaki) na Magomeni Kota, ambapo Benki ya CRDB, NMB, TIB na BOA Benki zimeshaonesha nia ya kutoa mkopo wa ujenzi, na mkopo kwa wanunuzi wa nyumba "Mortgage Financing" katika mfumo wa "Pre – Sale".

**Ukusanyaji wa Madeni ya TBA**

20. Mheshimiwa Spika, katika m w a k a wa fedha 2023/24 TBA iliingia na deni lenye jumla ya Shilingi bilioni 14.35. Kutokana na jitihada kubwa zilizofanywa na Wizara kupitia TBA katika kipindi tajwa, TBA imefanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 4.3. Hii ni sawa na 30% ya malimbikizo ya deni. Hivyo, deni lililobaki ni Shilingi bilioni 10.05. Nitoe wito kwa wapangaji wote kuhakikisha kuwa wanalipa kodi za pango kwa wakati ili kuepusha usumbufu kwao na kwa TBA. TBA inaendelea na jitihada za kufuatilia ulipaji wa madeni hayo kwa kutumia dalali wa mahakama ili fedha hizo zitumike kukarabati nyumba zilizopo, na kujenga nyumba mpya ili kukidhi mahitaji yaliyopo.

21. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika ukusanyaji wa madeni ya TBA, kupitia zoezi hilo kuna baadhi ya wadaiwa walikwazika. Ukusanyaji wa madeni hayo ni maelekezo ya Bunge letu tukufu na CAG, hivyo tunawaomba mtuvumilie wakati wa utekelezaji wa zoezi hilo kwani ni zoezi endelevu. Ni matarajio yangu kuwa baada ya kukamilika kwa zoezi hili TBA itaweza kuboresha huduma zake ili wapangaji wake wafurahie maisha bora ndani ya nyumba za TBA, na kujenga majengo mengi zaidi kulingana na mahitaji.

**Udhibiti Uzito wa Magari**

22. Mheshimiwa Spika, kuzuia uharibifu wa miundombinu ya barabara ni jambo la lazima na zoezi endelevu kwa kuwa tabaka la lami la barabara hujengwa kwa gharama kubwa.

i. Wizara ina mpango wa kufunga mizani yenye teknolojia inayopima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo (Weigh in Motion System), katika vituo vyote vya mizani nchini ili kutatua changamoto ya msongamano wa magari katika vituo vya mizani. Katika mwaka 2024/25 mizani 32 itajengwa. Lengo ni kuwa na jumla ya mizani 110 ifikapo mwaka 2026/27. Mizani hii yenye teknolojia ya kisasa hufungwa barabarani ili kuchuja magari ambayo hayajazidi uzito na kuyaruhusu kuendelea na safari, hivyo msafirishaji hatalazimika kuingia katika kituo cha mzani endapo gari lake halitabainika kuzidi uzito katika mizani ya WIM.
Mizani ya aina hii itasaidia kwa sehemu kubwa kupunguza msongamano wa magari barabarani na katika vituo vya mizani, na kupunguza muda wa safari kwa magari yaliyobeba mizigo inayokwenda nje ya nchi (Transit Vehicles) na ndani ya nchi, na hivyo kuendelea kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi.

ii. Wizara ya Ujenzi kupitia TANROADS ilianzisha na kutekeleza utaratibu wa magari ya mafuta (fuel tankers) na makasha yenye rakili (sealed containers) kupima uzito katika vituo 3 tu vya mizani katika kila ushoroba. Utaratibu huu umesaidia kupunguza muda wa safari pamoja na msongamano wa magari katika vituo vya mizani.

iii. Wizara imefanya marekebisho katika maeneo hatarishi yaliyopo barabara kuu ya kwenda Zambia, ili kupunguza ajali za barabarani; eneo la Mlima Kitonga lenye urefu wa km 7.6 kwa kufanya upanuzi wa kona 5 zenye urefu wa km 1.6 na upana wa mita 5. Ujenzi utaendelea kwa awamu hadi Mlima wote wa Kitonga upitike bila shida yoyote. Ujenzi wa maeneo ya maegesho, barabara za dharura na barabara ya mchepuo, yenye urefu wa km 2.8 kwa kiwango cha lami umefanyika ili kutenganisha malori na magari mengine katika eneo la Inyala mkoani Mbeya.

23. Mheshimiwa Spika, hayo ni machache kati ya mengi mazuri ambayo Serikali ya Awamu ya 6, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeyafanya katika Sekta ya Ujenzi. Hakika, Mheshimiwa Rais Samia /ni mama na Rais mwenye maono, muonesha njia na mchapakazi. Tunamuombea afya njema na maisha marefu ili aendelee kuiongoza Tanzania yetu kufikia mafanikio makubwa kijamii na kiuchumi.

**C. UHARIBIFU MKUBWA WA MIUNDOMBINU YA BARABARA NA MADARAJA KUTOKANA NA MVUA ZA EL-NINO NA KIMBUNGA HIDAYA**

24. Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeathirika na mabadiliko ya tabia nchi ambayo yameleta athari za kimazingira katika maeneo mbalimbali dunia nzima. Athari hizo kwa Tanzania zimejidhihirisha kupitia mvua kubwa za El – Nino zilizonyesha kwa takriban miezi 9 mfululizo kuanzia Septemba 2023 hadi hivi sasa mwezi Mei. Mvua hizo zimesababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara na madaraja kote nchini. Mikoa iliyoathiriwa zaidi ni Lindi, Ruvuma, Morogoro, Singida, Tabora, Dodoma, Kilimanjaro, Songwe, Simiyu, Mbeya, Rukwa, Mwanza, Dar es Salaam, Pwani, Arusha, Njombe, Iringa, Mtwara, Shinyanga na Manyara.

25. Mheshimiwa Spika, vilevile, kimbunga Hidaya kiliyakumba maeneo ya pwani ya nchi yetu na kusababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu katika mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani. Mvua kubwa zilizoambatana na kimbunga hiki, zilisababisha kukatika kwa mawasiliano baina ya mikoa ya Pwani na Lindi eneo la Mikereng'ende, Songas, Somanga na Matandu – Nangurukuru. Maeneo mengine yaliyoathirika kwa kiasi kikubwa ni katika barabara ya Nangurukuru – Liwale (daraja la Miguruwe, eneo la Zinga na eneo la Mlowoka); Kiranjeranje – Namichiga (daraja la mto Mbwemkuru na daraja la Kigombo) pamoja na Tingi – Kipatimu (eneo la mto Liomanga na eneo la mto Chumo).

Kwa ujumla, uharibifu uliotokea katika barabara ya Mtwara – Lindi – Dar es Salaam ni mkubwa, na hivyo barabara yote inatakiwa kujengwa upya. Tayari manunuzi kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa kipande cha barabara ya Mtwara - Mingoyo yapo katika hatua za mwisho, na ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Julai 2024.

26. Mheshimiwa Spika, Serikali ilichukua hatua za haraka kuhakikisha kuwa mawasiliano katika maeneo yaliyoathirika yanarejea. Hadi Mei 2024 kiasi cha Shilingi bilioni 72 zilitolewa kwa ajili ya kurejesha mawasiliano. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha za dharura. Tathmini ya jumla iliyofanyika imeonesha kuwa mahitaji halisi kwa ajili ya miundombinu iliyoathirika na mvua za El – Nino na Kimbunga Hidaya ni Shilingi trilioni 1.07. Serikali inasubiri taarifa ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kuhusu kumalizika kwa msimu wa mvua, kwa ajili ya kuendelea na ukarabati na matengenezo ya maeneo yaliyoathiriwa.

**D. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24**

Ushiriki wa Wazawa (Local Content) katika Utekelezaji wa Miradi Mikubwa ya Ujenzi

27. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Ujenzi ni mojawapo ya Sekta muhimu zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa. Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, wastani wa mchango wa Sekta katika Pato la Taifa katika kipindi cha miaka kumi (2012 – 2022) ni 14%. Sekta hii imekuwa ikikua kwa wastani wa 12% kwa mwaka kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita. Serikali imekuwa ikitenga fedha nyingi kila mwaka kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Miradi hiyo hutekelezwa na makandarasi kutoka ndani na nje ya nchi. Hata hivyo, pamoja na kutengewa kiasi kikubwa cha fedha, uchambuzi wa taarifa za usajili wa miradi ya ujenzi kwa miaka 10, (2013 – 2023), umebaini ushiriki mdogo wa makandarasi wazawa katika miradi hiyo.

28. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), kati ya jumla ya miradi 36,839, Wazawa walitekeleza miradi 35,351 sawa na asilimia 95.9 ya miradi hiyo katika kipindi cha 2013 - 2023. Hata hivyo, miradi iliyotekelezwa na wazawa ni midogo midogo yenye thamani ya Shilingi trilioni 23.749, sawa na 38.5% ya thamani ya miradi yote iliyosajiliwa na kutekelezwa katika kipindi cha miaka 10, ambayo ni Shilingi trilioni 61.638. Hivyo, makandarasi wa nje ambao ni takriban asilimia 4.1 walitekeleza miradi michache lakini yenye thamani kubwa ( yaani 61.5% ya thamani ya miradi yote).

Hii inaonesha kuwa asilimia kubwa ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inawanufaisha wageni kutoka nje ya nchi kuliko Wazawa. Sababu kubwa inayochangia hali hii ni uwezo mdogo wa makandarasi wa ndani wa kifedha, mitambo na wataalam; hivyo inakuwa vigumu kwao kushindana kwenye zabuni za kazi na makandarasi kutoka nje.

29. Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizi za makandarasi wa ndani, Wizara imedhamiria kuwawezesha makandarasi wazawa kushiriki kwenye kazi kubwa za ujenzi kuanzia usanifu, manunuzi, ujenzi, matengenezo na ukarabati. Uwezeshaji wa wazawa utaleta manufaa ikiwemo kukuza biashara za wazawa; kupunguza matumizi ya fedha za kigeni; kuongeza ajira na ujuzi kwa wataalam wa ndani, pamoja na kujenga uwezo wa kampuni za ndani kuweza kushindana kimataifa.

30. Mheshimiwa Spika, tarehe 21 Novemba, 2023 niliitisha mkutano wa mashauriano na makandarasi pamoja na washauri elekezi wa ndani kutoka mikoa yote Tanzania Bara na Zanzibar. Lengo la mkutano huo lilikuwa kupata maoni na ushauri kutoka kwa makandarasi wenyewe, kuhusu changamoto walizonazo na utayari wa Serikali kuzitafutia suluhu. Baada ya mkutano huo, niliunda timu ya wataalam ili wachambue changamoto hizo na kuandaa Mkakati wa Kuongeza Ushiriki wa Wazawa katika Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi (Local Content Strategy). Timu hiyo tayari imekamilisha kazi na imeandaa mapendekezo ya kufanyiwa kazi ya muda mfupi, wa kati na muda mrefu. Mapendekezo hayo ni pamoja na:

i. Kurekebisha vipengele kwenye makabrasha ya zabuni za TANROADS ambavyo vina masharti magumu bila sababu za msingi, na kusababisha wazawa washindwe kuvitimiza wakati wa kuomba zabuni, na hivyo kuondolewa kwenye mchakato wa zabuni;

ii. Serikali kuanzisha mpango maalum wa kuwajengea uwezo na kuwaendeleza makandarasi na wataalam wa ndani. Lengo ni kuwawezesha wakue na wawe na uwezo wa kushindana na makandarasi wa nje, hata kuwa na uwezo wa kuomba kazi nje ya nchi na hivyo kupanua wigo wa ajira kwa watanzania; na

iii. Sheria ya Manunuzi ya Umma kuboreshwa ili iongeze kiasi cha fedha kwa miradi ya kutekelezwa na wazawa peke yao kutoka kiasi cha Shilingi bilioni 10 cha sasa hadi Shilingi bilioni 50.

31. Mheshimiwa Spika, hadi Mei 2024 tayari Serikali imetekeleza mapendekezo hayo kwa kufanya yafuatayo:

i. TANROADS kwa kushirikiana na PPRA wanaendelea na taratibu za kuboresha/kurekebisha vipengele kwenye makabrasha ya zabuni vilivyokuwa vikwazo kwa makandarasi wazawa;

**Vipengele vilivyoboreshwa ni pamoja na:**

Kupunguza kiwango cha mapato ghafi (Average Annual Turnover);

a) Kutumiwa kwa Tender/ Bid Securing Declaration badala ya Tender/ Bid security;

b) Kutumia Performance Bonds/ Performance Securing Declaration badala ya Performance Bank Guarantee;

c) Kutambua uzoefu wa wataalam badala ya uzoefu wa kampuni kwa ajili ya kazi zinazofanana (specific experience in similar projects).

ii. Wizara imetenga miradi maalum ya kuwajengea uwezo makandarasi wa ndani na makandarasi wanawake; na

iii. Wizara ya Fedha imerekebisha Sheria ya Manunuzi ya Umma kwa kuongeza wigo wa thamani ya miradi ya kutekelezwa na wazawa peke yao. Imependekeza kiwango kipande kutoka Shilingi bilioni 10 za sasa hadi Shilingi bilioni 50. Nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, na Wizara ya Fedha anayoiongoza kwa ushirikiano wa karibu kwenye utekelezaji wa mikakati ya kuwezesha wazawa ambayo utekelezaji wake tumeanza mara moja.

32. Mheshimiwa Spika, sambamba na kuwajengea uwezo Makandarasi Wazawa, Wizara ina mkakati wa kuwajengea uwezo Makandarasi wanawake kwa kuongeza ushiriki wao katika miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara. Hadi sasa Wizara imetenga jumla ya kilometa 20 za ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kwa ajili ya Makandarasi wanawake pekee. Kazi hizi zitagawanywa katika sehemu za kilometa tano tano ambapo

Makandarasi wanawake pekee yao ndio wataomba kazi hizo. Hivi sasa miradi hii ipo kwenye hatua ya ununuzi.

33. Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa makandarasi wazawa kufanya kazi kwa weledi na utaalam, ili mikakati iliyowekwa na Serikali isitafsiriwe kama mteremko. Hii ni kwa kuwa baadhi ya makandarasi wazawa waliopewa miradi ya upendeleo wameikatisha tamaa Serikali kwa kutokuwa waadilifu, usimamizi usioridhisha wa miradi na kutumia muda mrefu katika utekelezaji wa miradi. Rai yangu kwa makandarasi wa ndani ni kushiriki kikamilifu, kwa uzalendo na uadilifu mkubwa katika ujenzi wa taifa letu. Vilevile mjiepushe na vitendo vya rushwa, tekelezeni mradi kwa ubora uliotegemewa, ili kutoangusha dhamira hii njema ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuwainua kiuchumi. Kazi kwenu makandarasi wazawa.

34. Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze kwa dhati Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania Taifa Mary Chatanda kwa ufuatiliaji wa karibu kuhusu fursa hizi kwa makandarasi wanawake. Kujenga Uwezo wa Ndani ya Taasisi na Wastaafu

**Wabobezi Katika Usimamizi wa Miradi**

35. Mheshimiwa Spika, TANROADS inatumia Kitengo chake cha ndani cha Ushauri wa Kihandisi (TECU) katika usanifu na usimamizi wa miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja. Lengo ni kujenga uwezo wa taasisi zetu kusimamia miradi badala ya kutegemea wataalam nje. Hii imesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza gharama za usimamizi wa miradi pamoja na muda unaotumiwa katika ununuzi wa wahandisi washauri. TECU imeshiriki kwa mafanikio makubwa katika utekelezaji wa miradi kadhaa ya kimkakati, ikiwemo Mradi wa Uzalishaji wa Umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Njia 8 ya Kimara – Kibaha (km19.2), Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Geita, na ujenzi wa kiwanda cha sukari cha Mbigiri.

Vilevile, Wizara kupitia taasisi zake ERB na TANROADS inaandaa utaratibu wa kutumia wataalam wa ndani waliostaafu (retired but not tired) katika ujenzi na matengenezo ya barabara. TECU inaendelea kuwatumia wahandisi wabobezi waliostaafu katika usanifu na usimamizi wa miradi. Hii imesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza utegemezi wa wahandisi washauri kutoka nje. Jambo hili la kutumia wastaafu pia linatoa fursa kwa wataalam wanaochipukia na ngazi ya kati kujifunza kutoka kwa wastaafu wabobezi ambao wako nyumbani wakati ujuzi wao bado unahitajika katika ujenzi wa taifa letu.

**Upatikanaji wa Malighafi za Ujenzi**

36. Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa malighafi za ujenzi, ikiwemo changarawe, mchanga, na kokoto, Wizara ya Ujenzi inaendelea na mazungumzo na Wizara ya Madini. Mazungumzo hayo yanalenga kupata namna bora ya kutatua changamoto kubwa ya upatikanaji wa malighafi hizo. Changamoto kubwa ni uwepo wa vishoka wanaoshikilia maeneo yenye malighafi za ujenzi na kutoza fedha nyingi. Serikali haitasita kuwachukulia hatua kali wale wote watakaobainika kujihusisha na mchezo huo mchafu. Dhamira ya Wizara ni kuwa kwa kadri inavyowezekana maeneo hayo yamilikishwe TANROADS ili kuwezesha miradi mingi ya barabara kutekelezwa kwa wakati, na kupunguza gharama za ujenzi.

Nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati Mhe. Antony Mavunde, Waziri wa Madini kwa ushirikiano anaotupatia katika kuhakikisha kuwa malighafi za ujenzi zinapatikana kwa gharama nafuu na hivyo kupunguza gharama za miradi. Hii itawezekana iwapo TANROADS itakuwa na maeneo ya kuchimba madini ya ujenzi na kuondokana na hali ya sasa ya vishoka wanaopandisha gharama za ujenzi. Utekelezaji wa Miradi kwa Utaratibu wa Kushirikisha

**Sekta Binafsi (PPP)**

37. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miradi ya miundombinu hasa ya barabara na madaraja inaigharimu Serikali kiasi kikubwa cha fedha. Ili kuipunguzia Serikali gharama kubwa za utekelezaji wa miradi hiyo, Wizara imeanza kuishirikisha sekta binafsi kwa utaratibu wa PPP. Lengo la kutumia utaratibu huu ni kujenga miundombinu na inasaidia kutekeleza miradi kwa wakati. Katika miradi ya barabara, Serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya Kibaha – Chalinze – Morogoro – Dodoma (Expressway) yenye urefu wa kilometa 423.8 kwa mfumo wa kulipia (Toll Road System). Mradi huu umegawanywa katika sehemu 3 kama ifuatavyo:

i. Sehemu ya Kibaha – Chalinze (km 78.9), kazi inayoendelea ni uchambuzi wa Proposals (Evaluation of Technical & Financial Proposals) wa wawekezaji waliofaulu vigezo vya kupatiwa Request for Proposals ya kutekeleza mradi huu.

ii. Kwa sehemu ya Chalinze – Morogoro yenye urefu wa kilometa 84.9, Mshauri Elekezi yupo katika hatua za mwisho kukamilisha kazi ya Upembuzi Yakinifu.

iii. Kwa sehemu ya Morogoro – Dodoma (km 260) usanifu wa kina wa kawaida (Conventional Design) uko katika hatua za mwisho kukamilika. Usanifu utatumika kujenga Concept ya mradi wa PPP.

**Utekelezaji wa Miradi kwa Utaratibu wa EPC+F**

38. Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kutekeleza miradi 7 ya ujenzi wa barabara zenye jumla ya urefu wa kilometa 2,035 zenye kugharimu Shilingi trilioni 3.7 kwa utaratibu wa Engineering, Procurement, Construction and Finance (EPC+F). EPC+F ni mfumo wa utekelezaji wa miradi kwa kutumia makandarasi ambao wanahusika katika taratibu za kumpata mgharamiaji wa mradi kwa njia ya mikopo. Mfumo huu kwa nchi yetu ni mpya na lengo la kutumia mfumo huu ni kupunguza utegemezi wa fedha za ndani katika ujenzi wa barabara. Miradi hiyo 7 imeoneshwa katika Aya ya 40 ya kitabu cha Hotuba. Serikali inaendelea na mazungumzo na makandarasi kuhusu ugharamiaji wa miradi yote 7 ili kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa dhamira ya Serikali ya kutekeleza miradi hii ya EPC+F bado ipo palepale.

39. Mheshimiwa Spika, naomba sasa nieleze kwa muhtasari utekelezaji wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2023/24.

**Bajeti ya Matumizi ya Kawaida**

40. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/24, Wizara ya Ujenzi ilitengewa jumla ya Shilingi 48,395,392,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi 43,958,274,000.00 zilikuwa ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake na Shilingi 4,437,118,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi zake.
Hadi Aprili 2024 jumla ya Shilingi 48,665,781,258.75 zilikuwa zimetolewa na HAZINA kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

**Bajeti ya Miradi ya Maendeleo**

41. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/24, Wizara ilitengewa Shilingi 1,419,843,057,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 2,699,800,000.00 zilihamishiwa Wizara ya Uchukuzi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Viwanja vya Ndege. Hivyo, Wizara ya Ujenzi ilibakiwa na Shilingi 1,417,143,257,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Hadi Aprili 2024 fedha zilizopokelewa ni Shilingi 1,421,842,330,490.81 ya fedha zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/24

a. Miradi ya Barabara na Madaraja Iliyotekelezwa

42. Mheshimiwa Spika, maelezo kuhusu utekelezaji wa miradi ya barabara na madaraja yameoneshwa katika Aya ya 42 - 129 ya kitabu cha Hotuba yangu.

b. Miradi ya Barabara na Madaraja Iliyosainiwa Mwaka wa Fedha 2023/24

43. Mheshimiwa Spika, pamoja na utekelezaji wa miradi

inayoendelea, Serikali imeamua kutekeleza miradi mipya ya ujenzi wa barabara ili kuhakikisha wananchi wanatumia miundombinu bora ya barabara. Katika mwaka wa fedha 2023/24, mikataba ya ujenzi/ukarabati/usanifu wa miradi 25 mipya ya barabara, madaraja na mizani ilisainiwa. Miradi hiyo ni:

i. Maboresho ya miundombinu ya mabasi yaendayo haraka iliyojengwa katika Awamu ya Kwanza (Kimara – Kivukoni; Kawawa Gerezani na Kawawa- Morocco zenye jumla ya km 20.9). Maboresho yanahusisha ukarabati wa sehemu ya Obama Drive pamoja na barabara iendayo Stendi ya mabasi ya Kivukoni na barabara ya Msimbazi;
ii. Ujenzi wa daraja la Simiyu (Wilaya ya Magu Mkoani Mwanza) (m 150) na barabara unganishi kilometa 3.0 kwa kiwango cha lami kwa utaratibu wa usanifu na ujenzi;
iii. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Tarime - Mugumu (km 86); Sehemu ya Tarime – Mogabiri (km 9.3), Nyamongo – Mugumu (km 48.15) pamoja na barabara ya kuelekea Mugumu Roundabout (km 3.6);
iv. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Bigwa – Matombo – Mvuha (km 78) pamoja na ujenzi wa daraja la Ruvu (m 64) na daraja la Mvuha (m 60);
v. Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Nachingwea – Ruangwa – Nanganga (km 106); sehemu ya Nachingwea – Ruangwa (km 57.6);
vi. Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Likuyufusi – Mkenda (km 122.5); sehemu ya Likuyufusi – Mhukuru (km 60);
vii. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kibada – Mwasonga – Tundwisongani Jct/Tundwisongani – Kimbiji (km 41); sehemu ya Kibada – Mwasonga (km 26.7) na Songani Jct – Kijata Jct;
viii. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ubena Zomozi - Ngerengere (km 11.6);
ix. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kitai – Lituhi (km 84.5); sehemu ya Ruanda – Ndumbi Port (km 50) kwa kiwango cha lami;
x. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ifakara– Kihansi (km 124); Sehemu ya Mbingu – Chita JKT (km 37.5);
xi. Ujenzi wa Mizani ya Kizengi pamoja na uwekaji taa za barabarani katika barabara ya Tabora - Nyahua – Chaya;
xii. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Iringa (Ipogolo) - Kilolo (km 33.61);
xiii. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya KongwaJct – Ngambi – Mpwapwa (km 32) na Mpwapwa - Gulwe - Kibakwe (km 46.9);
xiv. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kagwira – Ikola – Karema Port (km 112); Sehemu ya Kagwira – Kasekese (km 54.15);
xv. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kagwira – Ikola – Karema Port (km 112); Sehemu ya Kasekese - Ikola (km 56.91);
xvi. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Same - Kisiwani - Mkomazi (km 100.5); sehemu ya Lot 2: Ndungu – Mkomazi (km 36);
xvii. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Isongole II – Kasumulu – Ipyana – Katumbasongwe (km 114.3) ikijumuisha barabara ya Ndembo – Isoko Spur Road (km 5.92) na sehemu ya Muungano – Ipyana (km 0.66); Lot 1: Isongole II – Ndembo (km 46) na Ndembo Spur Road (km 6);
xviii. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Katumba – Mbambo - Tukuyu (km 79.4); sehemu ya Lot 3 : Katumba– Lupaso (km 35.3);
xix. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Katumba – Mbambo – Tukuyu (km 79.4); sehemu ya Lot4: Mbaka – Kibanja (km 20.7);
xx. Usanifu na ujenzi kwa kiwango cha lami (Design and Build) wa barabara ya Kyerwa - Omurushaka (km 50);
xxi. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Ntyuka Jct - Mvumi - Kikombo Jct (km 76) na Chololo - Mapinduzi (TPDF HQ) (km 5); sehemu ya Ntyuka – Mvumi Hospital - Kikombo (km 53);
xxii. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Kahama – Bulyanhulu Jct – Kakola (km 73);
xxiii. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50.6); sehemu ya Tatanda – Kasesya (km 25);
xxiv. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Dareda – Dongobesh (km 60); sehemu ya Dareda Mjini – Dareda Mission (km 8);na
xxv. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Sungusila – Nzera – Nkome Port (km 20.36).

44. Mheshimiwa Spika, maelezo ya utekelezaji wa miradi matengenezo ya barabara na madaraja, vivuko, nyumba na majengo ya TBA, pamoja na udhibiti wa uzito wa magari yameoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia Aya ya 133 – 150.

c. Miradi ya Ujenzi wa Miundombinu ya Viwanja vya

Ndege

45. Mheshimiwa Spika, majukumu ya ujenzi wa viwanja vya ndege nchini yamerejeshwa Wizara ya Uchukuzi. Hata hivyo, Wizara kupitia TANROADS inaendelea kutekeleza miradi ya uendelezaji wa viwanja vya ndege ambayo utekelezaji wake umefikia asilimia 40 na zaidi na miradi ambayo ina ufadhili wa Washirika wa Maendeleo. Miradi hiyo ni viwanja vya ndege vya Msalato, Geita, Kigoma, Tabora, Songwe, Mtwara, Sumbawanga, Shinyanga, Iringa, Musoma, Songea, Tanga na Lake Manyara. Miradi hii ikikamilika viwanja vitarejeshwa TAA kwa ajili ya usimamizi na uendeshaji.

Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi ya Viwanja vya Ndege yameoneshwa kwa kina katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia Aya ya 151 – 159.

**E. CHANGAMOTO ZILIZOIKABILI WIZARA NA MIKAKATI YA KUZITATUA**

46. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, zipo changamoto kadhaa ambazo zimechangia kutokufikiwa malengo kwa ufanisi uliokusudiwa. Changamoto hizo na mikakati ya kuzitatua zimeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu Aya ya 230.

**F. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25**

47. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi imeandaa Makadirio ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25 kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:

a) Kufanya matengenezo ya miundombinu ya barabara na madaraja iliyoharibiwa na mvua za El Nino na Kimbunga Hidaya. Serikali inaendelea na majadiliano na wadau wa maendeleo wakiwemo WB na AfDB ili kupata fedha za matengenezo kupitia dirisha la dharura la Contingency Emergency Response Component (CERC). Kipaumbele kitakuwa ni kurejesha miundombinu ya madaraja na makalavati katika maeneo yaliyoathiriwa nchi nzima.
b) Kuendelea na utekelezaji wa miradi inayoendelea ambayo ni pamoja na:

i. Ujenzi wa barabara za kimkakati zenye kufungua fursa za kiuchumi kama utalii, kilimo, madini, bandari, viwanda, Bwawa la Kufua Umeme la Nyerere;
ii. Miradi ya kupunguza msongamano katika miji mikubwa kama vile Jiji la Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Dodoma;
iii. Ujenzi wa barabara zinazounganisha makao makuu ya mikoa, zinazounganisha na nchi jirani kwa kiwango cha lami pamoja na barabara za ulinzi;
iv. Usanifu wa barabara mpya hasa mijini kwa kuzingatia mahitaji ya watumiaji wote wa barabara ikiwemo wanamichezo, watembea kwa miguu na wanaoendesha vyombo visivyo vya moto husus baiskeli;
v. Miradi ya kimkakati ikiwemo kukamilisha ujenzi wa viwanja vya ndege vya Msalato, Geita, Kigoma, Tabora, Songwe, Mtwara, Sumbawanga, Shinyanga, Iringa, Musoma, Songea, Tanga na Lake Manyara;
vi. Miradi ya udhibiti wa uzito wa magari ikiwemo kujenga mizani ya Weigh in Motion (WIM) ili kupunguza msongamano wa malori barabarani na kwenye mizani;
vii. Miradi ya ujenzi na ukarabati wa vivuko kupitia TEMESA; na
viii. Miradi ya nyumba na majengo ya Serikali kupitia TBA.

c) Kuendelea na matengenezo ya barabara Kuu na za Mikoa pamoja na madaraja kwa kuwatumia makandarasi wa ndani kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara pamoja na kuhakikisha kuwa barabara zinapitika katika majira yote ya mwaka;
d) Kuendelea kuwajengea uwezo wataalam wa ndani kupitia programu mbalimbali kwa lengo la kuongeza wataalam wabobezi wa ndani ili waweze kusimamia miradi mikubwa inayoendelea kutekelezwa nchini (Local content). Hii ni pamoja na kukijengea uwezo Kitengo cha Ushauri Elekezi wa Miradi cha TANROADS (TECU) ili kiendelee kusimamia miradi mikubwa ya kimkakati;
e) Kufanya mapitio ya Sera ya Ujenzi (2003) na Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani (2009) pamoja na kanuni na miongozo mbalimbali inayohusiana na Sekta ya Ujenzi ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia na tabianchi;
f) Kuendelea kuimarisha utendaji kazi;
g) Kutumia teknolojia za gharama nafuu katika ujenzi wa barabara husus katika maeneo korofi;
h) Kutekeleza Mkakati wa Uimarishaji wa Utendaji kazi wa TEMESA (TEMESA Transformation Strategy 2024 – 2034).

**Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida**

48. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ya Ujenzi imetengewa Shilingi 81,407,438,000.00 ikiwa ni Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi 76,588,233,000.00 ni Bajeti ya Mishahara na Shilingi 4,819,205,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**Makadirio ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo**

49. Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Maendeleo kwa Wizara ya Ujenzi ni Shilingi 1,687,888,714,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 1,141,803,989,000.00 ni fedha za ndani na Shilingi 546,084,725,000.00 ni fedha za nje. Kati ya fedha za ndani, Shilingi 599,756,467,800.00 ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya Mfuko wa Barabara na fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali ni Shilingi 542,047,521,200.00.

Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyooneshwa katika Kiambatisho Na.1.

50. Mheshimiwa Spika, pamoja na miradi hiyo, Wizara kupitia TANROADS itaanza utekelezaji wa mradi wa kimkakati wa Ujenzi wa Daraja la Jangwani ambao ni sehemu ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa maendelezo ya Bonde la Mto Msimbazi. Daraja litakalojengwa lina urefu wa mita 390 pamoja na barabara unganishi zenye urefu wa mita 710 na kina cha mita 15.5 kutoka usawa wa bahari. Daraja hili litakapokamilika litatatua changamoto ya kujaa kwa maji katika barabara ya Dar es Salaam - Morogoro eneo la Jangwani wakati wa mvua na kusababisha kufungwa kwa barabara hiyo mara kwa mara. Tathmini ya zabuni ili kumpata Mkandarasi na Mhandisi Mshauri zinaendelea.

51. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ambayo inalenga kuondoa kero ya msongamano wa magari katika majiji. Miradi hiyo ni pamoja na

i. Upanuzi wa barabara ya Mwanza - Usagara – Daraja la JPM kuwa njia 4 (km 37): Sehemu ya Mwanza – Usagara (km 22);
ii. BRT Awamu ya 3: Mradi huu unahusisha barabara ya Nyerere kuanzia makutano ya barabara ya Kivukoni na Mtaa wa Azikiwe hadi Gongolamboto (km 23.33);
iii. BRT Awamu ya 4 (km 30.12): Mradi huu unahusisha barabara ya Ali Hassan Mwinyi – Morocco – Mwenge – Tegeta; na kipande cha Mwenge – Ubungo;
iv. BRT Awamu ya 5 (km 27.6): Mradi huu unahusisha barabara ya Mandela kuanzia makutano ya Ubungo – Bandari, makutano ya Mandela/Tabata – Tabata Segerea na Tabata – Kigogo;
v. Upanuzi wa barabara ya Mbagala Rangitatu - Kongowe (km 3.8) na daraja la Mzinga ili kupunguza ajali na kero kubwa ya foleni;
vi. Upanuzi wa barabara ya Mwai – Kibaki (Morocco – Shoppers Plaza – Kwa Nyerere – Kawe Roundabout – Africana: km 11.6);
vii. Upanuzi wa barabara ya Uyole – Ifisi - Songwe Airport Jijini Mbeya yenye urefu wa kilometa 36 kutoka njia 2 kuwa njia 4;
viii. Ukamilishaji wa ujenzi wa barabara ya mzunguko katika Jiji la Dodoma unaohusisha ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya mzunguko wa nje yenye jumla ya urefu wa kilometa 112.92 (Ihumwa Dry Port – Matumbulu – Nala: km 60.62); na (Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port: km 52.3);
ix. Ujenzi wa barabara hapa Dodoma ya mzunguko wa ndani (Bahi Round about – Image Round about – Ntyuka Round about na Makulu Round about: km 6.3);
x. Ujenzi wa barabara ya mzunguko wa kati hapa Dodoma (Nanenane – Miyuji – Mnadani Sekondari – Mkonze – Ntyuka – Nanenane : km 47.2);
xi. Upanuzi wa barabara ya Dodoma – Morogoro eneo la Bunge hadi Mji wa Serikali Mtumba; na
xii. Ujenzi wa barabara za mchepuo za Singida (Kisaki –

Kititimo – Mtipa – Manga: km 46), Iringa (Stendi ya Igumbilo – Kihesa Kilolo: km 7), Kilimanjaro (Kwa Sadala) na Songea (Namanditi – Changarawe: km14.4).

xiii. Ujenzi wa barabara za kupunguza msongamano mkoa wa Morogoro: Msamvu - Kinguluwila km 7; Msamvu- Kihonda km 5; na Msamvu – Mafiga km 3

**Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi**

52. Mheshimiwa Spika, miradi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, madaraja, viwanja vya ndege, vivuko na majengo inagharimu fedha nyingi na hivyo kuhitaji uwekezaji mkubwa. Ni dhahiri kuwa, Serikali pekee haitakuwa na uwezo wa kutekeleza miradi hii yote kwa wakati kutokana na ufinyu wa bajeti. Ili kuipunguzia Serikali gharama kubwa za utekelezaji wa miradi hiyo sambamba na kupunguza muda mrefu unaotumika katika kutekeleza miradi, Wizara inakaribisha ushiriki wa sekta binafsi kwa utaratibu wa PPP. Serikali imefanya maboresho makubwa katika Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (Sura 103) kwa lengo la kuvutia uwekezaji katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu. Maboresho haya yatasaidia kuhakikisha kuwa mazingira ya uwekezaji yanakuwa rafiki zaidi kwa wawekezaji wa ndani na wa kimataifa.

53. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya Kibaha – Chalinze – Morogoro – Dodoma Expressway kwa utaratibu wa PPP. Serikali inaandaa andiko la ujenzi wa barabara ya TANZAM (kwa toll road system ya utaratibu wa PPP), kuanzia Morogoro – Iringa – Mbeya hadi Tunduma kwa kuanzia na sehemu ya Igawa – Mbeya hadi Tunduma, ambayo kwa kiasi kikubwa itasaidia kupunguza msongamano wa magari katika mpaka wetu na Zambia pale Tunduma, na pia msongamano wa magari katika Jiji la Mbeya.

54. Mheshimiwa Spika, miradi mingine iliyoainishwa na Wizara ambayo inawezekana kutekelezwa kwa utaratibu wa PPP ni:

i. Barabara za Mzunguko Dar es Salaam:Outer Ring Road (Bunju – Kibamba – Pugu Kajiungeni – Mzinga – Tuangoma – Kigamboni :km 61); Middle Ring Road (Mbezi - Mbezi Mwisho – Kifuru – Banana – Kipara – Kigamboni : km 49); ii. Daraja la Pili la Kigamboni (Magogoni – Kivukoni) ambapo maandalizi ya kufanya upembuzi yakinifu wa awali yanaendelea; na

iii. Barabara ya Himo – Moshi – Arusha (Tengeru – km 78).

Wizara inawakaribisha wawekezaji wenye nia kushiriki katika utekelezaji wa miradi hii na mingine itakayoibuliwa kwa ajili ya kutekelezwa kwa njia ya ubia. Wizara imepanga kufanya mkutano mkubwa na wawekezaji kwa lengo la kutangaza na kujadiliana kuhusu namna bora ya kutekeleza miradi hii kwa utaratibu wa PPP. Mkutano huo umepangwa kufanyika mwezi Julai 2024. Waheshimiwa wabunge mnakaribishwa sana.

55. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya vivuko, kuna fursa mbalimbali katika uendeshaji wa vivuko hususan katika eneo la Kigamboni – Kivukoni. Kwa sasa, eneo la Kigamboni lina wakazi zaidi ya 300,000 ambapo wanaotumia usafiri wa kivuko ni wastani wa watu 60,000 kwa siku. Hata hivyo, kuna changamoto ya uchakavu wa vivuko vinavyohudumia katika eneo hilo, ambapo kwa sasa kivuko cha MV. Kazi pekee ndiyo kinafanya kazi kwa uhakika. Kivuko cha MV. Magogoni kinaendelea kufanyiwa ukarabati mkubwa. Kivuko cha MV. Kigamboni pia kipo katika matayarisho ya kufanyiwa ukarabati mkubwa. Hivyo, Serikali imeamua kushirikiana na Sekta Binafsi katika utoaji wa huduma za vivuko katika eneo hilo. Kwa sasa, TEMESA inashirikiana na Azam Marine Company Ltd kwenye utoaji wa huduma kivukoni hapo.

Wizara inaendelea kuangalia utaratibu bora zaidi wa ushirikiano huo ili kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na tija kwa pande zote mbili. Matarajio ya Wizara ni kuwa ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji huduma za vivuko katika eneo la Kigamboni utaondoa kero kwa wananchi wanaotumia huduma hiyo.
Nitoe wito kwa wawekezaji wengine wenye nia kushirikiana na TEMESA katika utoaji wa huduma za vivuko katika maeneo mengine nchini. Aidha, tunawakaribisha wawekezaji kuingia ubia (Joint Venture) na TEMESA katika matengenezo ya magari na ukodishaji wa mitambo.

56. Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kukemea taarifa za kupotosha zinazotolewa na vyombo vya habari kuhusu vivuko vya Kigamboni na kuzua taharuki kwa wananchi wa eneo hilo. Serikali ipo kazini na haiwezi kuhatarisha usalama wa raia wake kwa namna yoyote ile. Hivyo, niwaombe wananchi wa Kigamboni kuwa watulivu wakati Serikali inaendelea kuboresha huduma za vivuko pale Kigamboni, sambamba na maboresho ya barabara ya Kibada – Mwasonga Jct na Songani Jct – Kijata Jct yanayolenga kuifanya Kigamboni kuwa mji bora.

57. Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya nyumba, TBA ina jumla ya nyumba na majengo 7,116 Tanzania Bara. Licha ya uwepo wa nyumba hizi, bado uhitaji wa nyumba kwa watumishi wa umma (hata waheshimiwa wabunge) hapa Dodoma na wananchi wengine ni mkubwa ambapo inakadiriwa mahitaji halisi ni takriban nyumba milioni 3 nchi nzima. Katika kuongeza kasi ya uwekezaji katika nyumba, TBA imeweka mikakati mbalimbali ya kuongeza vyanzo vya fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi yake, ikiwa pamoja na kuboresha ushirikiano na sekta binafsi katika uendelezaji wa milki nchini.

Nitoe wito kwa wawekezaji wa ndani na wa kimataifa, taasisi za kifedha, na wadau wa maendeleo kuchangamkia fursa hizi adhimu zilizopo katika sekta ya ujenzi ili pande zote mbili, yaani Serikali na wawekezaji binafsi wafaidike.

**Matumizi ya Teknolojia Mpya**

58. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TANROADS itaendelea kufanya tafiti mbalimbali katika kubaini teknolojia mpya, nafuu na zenye tija katika miradi ya ujenzi. Maelezo ya kina kuhusu teknolojia hizo yameoneshwa katika Aya ya 224 – 225 ya Kitabu cha Hotuba ya Bajeti ya Wizara.

**Udhibiti wa Ubora wa Barabara**

59. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya kuharibika kwa barabara kabla ya muda wake, Wizara imepanga kuanza kutumia mitambo maalum ya kupima ubora wa barabara (Road Scanners). Matumizi ya teknolojia hii yatatuwezesha kupima ubora wa barabara kama X– ray inavyopima mwili wa binadamu. Wizara imeamua kutumia teknolojia hii ya kisasa ili kuondoa kabisa matumizi ya vifaa visivyostahili katika upimaji wa ubora wa barabara vinavyotumika kwa sasa. Hivyo sururu sasa basi. Matumizi ya mitambo hii yatadhibiti makandarasi wasio waaminifu wanaocheza na viwango vya ubora wa barabara wanazojenga. Mitambo iliyonunuliwa ina thamani ya Shilingi bilioni 5.1. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha za kununua mitambo hii.
Ushirikishwaji wa Makundi Maalum katika Kazi za Barabara

60. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kutekeleza mikakati ya kuwajengea uwezo makundi maalum hususan wanawake na vijana ili kuongeza ushiriki wao katika kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara nchini. Katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara kupitia ERB, CRB na AQRB itaandaa mpango mahsusi wa kuwajengea uwezo
vijana kwa nyenzo na ujuzi ili waanzishe kampuni za ujenzi na ushauri elekezi zitakazoshiriki katika ujenzi wa miundombinu. Wizara ina mpango unaofanana na BBT kiuhandisi, ambao utawajengea vijana kesho iliyo bora kwa kutenga miradi ambayo itawaongezea uzoefu katika kazi zao.

61. Mheshimiwa Spika, mikakati mingine inayotekelezwa na Wizara ni pamoja na kuendesha programu ya SEAP na EAPP kupitia ERB na AQRB mtawalia. Programu hizi zinalenga kuwapatia ujuzi na uzoefu wahandisi wahitimu pamoja na wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi ili waweze kusajiliwa kama wataalam (professionals). Vilevile, Wizara kupitia ICoT inaendesha mafunzo ya muda mrefu katika fani za ujenzi, umeme na mitambo katika ngazi za Astashahada na Stashahada ili kuzalisha wataalam watakaohudumia Sekta ya Ujenzi. Mafundi hawa ni muhimu sana katika utekelezaji wa kazi za ujenzi.

Vilevile ICoT inaendesha mafunzo maalum ya muda mfupi kwa makundi maalum ya vijana, wanawake, wazee na wasiojiweza ili kuwajengea uwezo wa kushiriki katika kazi za matengenezo ya barabara zinazotolewa na TANROADS na TARURA. Lengo la mafunzo yote ni kuongeza ushiriki wa makundi hayo muhimu katika shughuli za ujenzi wa barabara. Wahitimu wa mafunzo haya huweza kuunda kandarasi kupitia CRB na hivyo kukidhi vigezo vya kupatiwa kazi za matengenezo ya barabara.

Nitoe rai kwa makundi ya vijana na wanawake kurasimisha na kuingiza sokoni kazi zao ili kuchangamkia fursa hii adhimu inayotolewa na Wizara. Wizara inaahidi kuwasimamia kwa kuzingatia taaluma zenu na kuwalea hadi kuwa kampuni kubwa zenye uwezo wa kushindana katika soko.

**F. SHUKRANI**

62. Mheshimiwa Spika, kupitia hadhira hii, naomba kuwatambua na kuwashukuru Washirika mbalimbali wa Maendeleo pamoja na wadau wote ambao wameshirikiana nasi kwa namna moja au nyingine katika utekelezaji wa mipango mbalimbali ya Wizara. Kipekee nawashukuru wafuatao: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Japan (JICA), OPEC Fund, Korea Kusini (KOICA), Abu Dhabi Fund, Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Kuwait Fund, Barrick, EACOP, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za SADC, Japan, China, Norway, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF na PSSSF, Taasisi za fedha za CRDB, NMB, NBC na TCB na Asasi mbalimbali zisizokuwa za Serikali; Sekta Binafsi pamoja na wadau wengine wengi. Nawashukuru wadau hawa kipekee kwa kukubali kwa kauli moja kushirikiana na Serikali katika utekelezaji wa mkakati wa kuongeza ushiriki wa wazawa katika miradi ya ujenzi. Niseme tu kwamba asanteni sana.

63. Mheshimiwa Spika, naomba nitoe tena shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara (www.mow.go.tz).

**G. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UJENZI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2024/25**

64. Mheshimiwa Spika, fedha ninazoziomba pamoja na masuala mengine zitatumika kutekeleza kazi zifuatazo;

i. Kukamilisha miradi ya barabara 12 ambayo utekelezaji wake umefikia asilimia 70 au zaidi kama inavyooneshwa katika Aya ya 17 ya Kitabu cha Hotuba yangu;

ii. Kuendelea na miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja 62 ambayo utekelezaji wake upo chini ya asilimia 70 lakini kazi zinaendelea (Aya ya 17 ya Kitabu cha Hotuba); na

iii. Kutekeleza miradi ya majengo ya Serikali, vivuko, karakana na viwanja vya ndege.

65. Mheshimiwa Spika, katika mwaka w a fedha 2024/25, Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Trilioni moja, Bilioni mia saba sitini na tisa, Milioni mia mbili tisini na sita, Mia moja hamsini na mbili elfu (1,769,296,152,000.00) kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni themanini na moja, Milioni mia nne na saba, Mia nne thelathini na nane elfu (81,407,438,000.00) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara na Taasisi na Shilingi Trilioni moja, Bilioni mia sita themanini na saba, Milioni mia nane themanini na nane, Mia saba kumi na nne elfu (1,687,888,714,000.00) kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, Shilingi Bilioni sabini na sita, Milioni mia tano themanini na nane, Mia mbili thelathini na tatu elfu (76,588,233,000.00) ni za Mishahara ya Watumishi na Shilingi Bilioni nne, Milioni mia nane kumi na tisa, Mia mbili na tano elfu (4,819,205,000.00) ni za Matumizi Mengineyo.

Bajeti ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inajumuisha fedha za ndani Shilingi Trilioni moja, Bilioni mia moja arobaini na moja, Milioni mia nane na tatu, Mia tisa themanini na tisa elfu (1,141,803,989,000.00) na fedha za nje ni Shilingi Bilioni mia tano arobaini na sita, Milioni themanini na nne, Mia saba ishirini na tano elfu (546,084,725,000.00). Fedha za ndani zinajumuisha Shilingi Bilioni mia tano tisini na tisa, Milioni mia saba hamsini na sita, Mia nne sitini na saba elfu na mia nane (599,756,467,800.00) kutoka Mfuko wa Barabara na Shilingi Bilioni mia tano arobaini na mbili, Milioni arobaini na saba, Mia tano ishirini na moja elfu na mia mbili (542,047,521,200.00) ni fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali.

66. Mheshimiwa Spika, pamoja na Hotuba hii, nimeambatisha mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa na Wizara katika mwaka wa fedha 2024/25 (Kiambatisho Na. 1 – 5). Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja yangu.

***67. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.***



# Mbwa, paka wafungwa kizazi kudhibiti ongezeko

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kupunguza tatizo la uzururaji mitaani kwa mbwa na paka wizara inayohusiana na masuala ya mifugo, imeanzisha utaratibu wa kuwafunga kizazi wanyama hao ili kupunguza idadi ya kuzaliana.

Pia, imewapatia chanjo dhidi ya maradhi hatari yanayoweza kusababisha vifo kwa binaadamu.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Waziri huyo alikuwa akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2024-2025.

Khamis alisema kumekuwepo na ongezeko kubwa la wanyama hao ambao wapo wanaofugwa na binadamu na wengine kuzurura ovyo mitaani na kutishia maisha ya binadamu.

**Hadi sasa Zanzibar inaingiza nyama ya kitoweo ikiwemo ngombe kwa asilimia 80 kutoka Tanzania Bara.**

Alisema mbwa 50 pamoja na paka 350 wamefungwa uzazi ili kupunguza tatizo hilo.

Aidha, alisema mbwa wasipopata chanjo kwa wakati wanaweza kusababisha maradhi makubwa ikiwemo kichaa cha mbwa ambacho ni hatari kwa afya binadamu na kusababisha kifo.

Alisema yapo baadhi ya maeneo ambayo mbwa wazururaji ni wengi mitaani na hivyo kuwa tishio kwa afya ya binadamu zaidi katika maeneo yaliyoshamiri sekta ya utalii.

"Mheshimiwa Spika tumeanza zoezi la kuwafunga uzazi mbwa pamoja na paka ili kuepusha tatizo la uzururaji ovyo ambapo wito wetu kwa wafugaji kupeleka mifugo yao kupata chanjo inayostahiki ili kuwaweka katika mazingira mazuri ya afya" alisema.

Hata hivyo alisema kwa mwaka wa fedha 2024-2025 wizara yake imejipanga kuimarisha kazi za utafiti wa mifugo kwa ajili ya kuongeza idadi kubwa ya wanyama kwa ajili ya matumizi ya kitoweo.

Alisema hadi sasa Zanzibar inaingiza nyama ya kitoweo ikiwemo ngombe kwa asilimia 80 kutoka Tanzania Bara.

Hivyo, aliliomba Baraza la Wawakilishi kuidhinisha Sh.bilioni 128.1 kwa ajili ya kazi za kawaida na maendeleo, huku taasisi ya utafiti ikipewa kipaumbele katika kufanya kazi za utafiti katika sekta ya umwagiliaji maji na mifugo.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na utalii, Hussein Ibrahim Makungu, alisema wanaunga mkono hatua za kuwafunga uzazi wanyama hao ambao idadi yao ikiongezeka.

Alisema wanyama hao wanatakiwa kudhibitiwa zaidi katika maeneo ya ukanda wa utalii ili kuepuka athari za kuwashambulia wageni na kusababisha madhara makubwa.

## Dk. Mwinyi aikaribisha Ufaransa kuwekeza Z'bar

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi ameikaribisha Ufaransa kuja Zanzibar kuangalia fursa za uwekezaji kwenye sekta za utalii, uvuvi na ufugaji wa vifaranga vya Samaki.

Pia, ameikaribisha katika uwekezaji wa Bandari, mafuta na gesi pamoja na sekta ya usafirishaji wa majini.

Aliyasema hayo visiwani hapa wakati wa kongamano la kwanza la biashara lililojumuisha wadau wakubwa wa biashara na wawekezaji, wamiliki wa viwanda kutoka Ufaransa na Jumuiya za Wafanyabiashara wa Zanzibar.

Dk. Mwinyi aliueleza ugeni huo ulioongozwa na Balozi wa Tanzania nchini Ufaransa, Ali Jabir Mwadini pamoja na Balozi wa Ufaransa nchini, Nabil Hajlaoui kwamba utalii wa Zanzibar una mchango mkubwa kwa uchumi wa nchi.

Alisema, utalii unaochangia asilimia 30 ya pato la taifa ambao unajumuisha utalii wa fukwe, urithi, michezo, pamoja na utalii mpya wa afya na mikutano ya kimataifa.


Dk. Mwinyi aliwaeleza wafanyabiashara na wawekezaji hao kutoka Ufaransa kwamba Zanzibar pia imejikita kwenye sekta ya uchumi wa buluu, ambayo imejipambanua kwenye maeneo muhimu yakiwemo uvuvi na ufugaji wa vifaranga vya samaki, ukulima wa mwani na utalii.

Pia alisem sekta ya Uvuuvi na ufugaji wa samaki, hutoa fursa nyingi kwa wavuvi na ajira za mtu mmoja mmoja wanaojihusisha na shughuli za maboti na majahazi, kilimo cha mwani kilichobeba asilimia kubwa ya kinamama wanaoongoza kuzalisha mwani mzuri Afrika.

Dk. Mwinyi alisema Zanzibar inanufaika na sekta ya bandari zikiwemo bandari jumuishi ya Mangapwani iliyo kwenye matengenezo makubwa, yenye nia ya kusafirisha na kuingiza makontena ya wafanyabiasaha walio wengi wa ndani na nje.

Alisema Bandari ya Malindi, Mkokotoni na Fumba zinaendeleza uchumi wa nchi ili kukidhi mahitaji ya uchumi wa watu kama vituo muhimu vya usafirishaji, usambazaji wa bidhaa.

Alisema sekta hiyo pia inaimarisha biashara na uchumi kupitia Bandari za Zanzibar, Pemba, Tanga, Dar es Salaam na Mtwara kusafirisha maeneo mengine ikiwemo Msumbiji, visiwa vya Comoro.



Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum (kulia), akijadiliana jambo na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wenye Ulemavu, Salma Saadati, baada ya kumaliza mkutano wa jukwaa la kitaifa la kimkakati na midahalo ya kiuchechemuzi kwa asasi za kiraia, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Asasi za kiraia zatakiwa kufuatilia mipango ya maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum amezitaka asasi za kiraia Zanzibar, kufuatilia mipango ya maendeleo na kuzitumia fursa zilizopo ili kushirikiana na serikali katika kutekeleza miradi.

Aliyasema hayo jana visiwani hapa wakati akizungumza katika Jukwaa la Kitaifa la Kimkakati na Midahalo ya Uchechemuzi kwa Asasi za Kiraia Zanzibar.

Dk. Mkuya alisema Serikali ya Zanzibar inafahamu mchango wa asasi za kiraia ambazo uwakilishi wake ni mkubwa kwa jamii.

Alisema serikali imeahidi kuzishirikisha asasi za kiraia katika mpango wa ujenzi wa taifa ikiwemo katika Bajeti Kuu ya Serikali na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2024-2025 ili maoni ya wananchi kusikika kikamilifu na kufanyiwa kazi.

Aidha, alisema huu ni wakati muafaka kuona kwamba mchango wa asasi za kiraia katika ujenzi wa taifa unapatikana kwa sababu jumuiya hizo zinawakilisha maoni ya wananchi katika ujenzi wa taifa.

Dk. Mkuya alisema anataraa kuwasilisha Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024-2025 Juni 13 ambayo itatanguliwa na Mpango wa Taifa wa Maendeleo na Uchumi.

Hivyo, alizitaka asasi hizo kushiriki kutoa maoni yao kwenye bajeti hiyo na mpango wa maendeleoili kutoa mawazo tofauti na ari mpya katika utekelezaji wa maoni ya kitaifa.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu (JUWAUZA), Salma Sadati alisema wakati umefika kuona asasi za kiraia zinafanya kazi na serikali katika ujenzi wa taifa.

Aliitaka serikali kutambua mchango wa asasi hizo katika ujenzi wa taifa kutokana na ushiriki wake mkubwa wa wananchi, ambapo serikali inatakiwa kuwa tayari kuzisaidia asasi hizo ambazo nyingi zinaishi kwa fedha za miradi ya washiriki wa maendeleo.

Mtaribu wa mradi wa uraia wetu unaotekelezwa na JUWAUZA, Selemani Baitani alisema asasi za kiraia zinakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo upatikanaji wa ruzuku na ulazima wa ulipaji wa ada za wanacahma kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) na changamoto za kodi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**BERNADETHA K PAUL** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S1442-0508** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MWANDET SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019 na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3777-0004** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **WINAM CAREER SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016 na pia Transcript na cheti cha chuo vyenye usajili namba **TU/DARCO/BHRM/019/150** vilivyotolewa na **TUMAINI UNIVERSITY** mwaka 2022. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/94795/2024, PHQ/DAR/UBU/87638/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**NTIGUMIGWA JUMA MKUYU** anatangaza kupotea kwa cheti cha **DIPLOMA IN PHARMACEUTICAL NTA L-6** chenye usajili namba **NS1571/0102/2015** kilichotolewa na **APPLE VALLEY INSTITUTE OF HEALTH SCIENCE** mwaka 2023. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIG/101549/2024**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**THERESIA AISHA MEREI** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba **AB370236** iliyotolewa DAR ES SALAAM PCO. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarif kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/KIL/RB/3631/2022**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI NA PIKIPIKI

**ELADIUS ROGATH MUSHY** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA NOAH** yenye usajili namba **T 845 CVR** na kadi za pikipiki aina ya **BOXER na TVS** zenye namba za usajili **MC 574 CVN na Mc 956 CTT.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DA/KIN/102077/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**OMARI ALLY ATHUMANI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC386EAL** aina ya **TVS,** Chassis No. **MD6254F42P1E07280,** Engine No. **DF4EP1606161.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/20816/2024**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU DODOMA**

**SHAURI LA MADAI NA. 48 YA 2023**

**GREYSON MPANDA ......................................MDAI**

**DHIDI YA**

**RAHEL DANIEL....................................MDAIWA**

**KWA: RAHEL DANIEL**
**POPOTE PALE ALIPO**

**YAH: TAARIFA YA KUTAJWA KWA SHAURI LA MADAI NA.48 YA 2023**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA.**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu litatajwa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma mbele ya **MHE. E. E. KAKOLAKI,** JAJI wa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma , saa tatu (3:10) asubuhi siku ya Jumanne tarehe 23/7/2024.
**HIVYO;** Unatakiwa Ufike wewe wenyewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa .
**NA ENDAPO;** Hutofika wewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakanyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo.
**IMETOLEWA;** Kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 22/05/2024.

NAIBU MSAJILI
DODOMA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya MOROGORO**

**Kituo cha MJINI Mkoa MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi Na 25/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU OMARY HASSANI WA MJI MPYA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA AISHA OMARY**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 10 mwezi 06 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo
**Zingatia;**
Endapo kuna mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa
Imetolewa leo tarehe 8 mwezi 5 mwaka 2024

Hakimu

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Marekani yasema Israel haijavuka mstari hatari

**NEW YORK,** MAREKANI

SERIKALI ya Marekani imesema bado haiamini kwamba jeshi la Israel limeanzisha uvamizi kamili katika mji wa Rafah kusini mwa Ukanda wa Gaza.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Msemaji wa Ikulu, John Kirby, saa chache baada ya vikosi vya Israel kufika katikati mwa mji huo na kuripotiwa kukamata kilima muhimu kimkakati kinachotazamana na mpaka wa karibu na Misri.

Rais wa Marekani Joe Biden alisema hapo awali kuwa uvamizi katika mji wa Rafah, ambao unahifadhi maelfu ya raia utavuka mstari mwekundu.

Kirby pia alihojiwa kuhusu shambulizi la anga la Israel na kusababisha moto ulioua Wapalestina 45 katika kambi moja ya watu waliokimbia makazi yao siku ya Jumapili.

Israel ilisema inaamini kuwa moto huo unaweza kusababishwa na silaha zilizohifadhiwa na Hamas katika maeneo ya jirani kulipuka.

Msemaji huyo aliwaambia waandishi wa habari kwamba picha za shambulio hilo ambalo liliua wanawake wengi, watoto na wazee, limevunja moyo na la kutisha.

„Hapapaswi kuwa na maisha yasiyo na hatia yanayopotea hapa kutokana na mzozo huu," aliongeza.

Lakini alikiri kuwa Israel inachunguza tukio hilo na kusema hakuna mabadiliko ya kisera anayoweza kuzungumza kufuatia matukio ya hivi karibuni huko Rafah.

„Bado hatuamini operesheni kubwa ya ardhini inafaa na hatujaona hilo kwa wakati huu," alisema.

Rais Biden alisema mapema mwezi huu kwamba baadhi ya usambazaji wa silaha kwa Israel utasitishwa iwapo kutakuwa na operesheni kubwa ya ardhini katika mji huo.

Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu alielezea shambulio hilo kama la bahati mbaya, huku akiapa kuendeleza operesheni ya Rafah.

Jeshi la Israel lilisema shambulio hilo lililenga na kuwaua maafisa wawili wakuu wa Hamas.

Lilisema wanajeshi wake walikuwa wakiendelea na shughuli kazi katika maeneo ya magaidi ndani ya Rafah.

Walioshuhudia walisema vifaru vya Israel vilikuwa vinazunguka eneo la al-Awda,

Baadhi ya wakazi walisema maeneo ya Magharibi ya mji huo yalikumbwa na mashambulizi makali ya mabomu usiku wa kuamkia Jumatatu na jumanne. Jeshi la Israel limekanusha ripoti iliyotolewa Jumanne kwamba mizinga ya vifaru vyake vilipiga kambi nyingine ya mahema katika eneo la al-Mawasi, iliyoko pwani ya magharibi ya Rafah, ambayo maafisa wa eneo hilo walisema watu 21 waliuawa.

Video za tukio hilo zilizochapishwa kwenye mitandao ya kijamii na kuchambuliwa na BBC Verify zilionyesha watu wengi wakiwa na majeraha mabaya.

Hakukuwa na dalili za wazi ya eneo la mlipuko, na hivyo kufanya kutowezekana kufahamika sababu ya tukio hilo.

*BBC*




Rais Cyril Ramaphosa na mkewe Tshepo Motsepe, wakishiriki upigaji kura katika kituo cha Chiawelo kwenye kitongoji cha Soweto jana. **PICHA: REUTERS**

# Afrika Kusini kuamua nani atakuwa rais

**PRETORIA,** AFRIKA KUSINI

RAIA wa Kusini jana wamepiga kura ya kuwachagua wabunge katika uchaguzi ambao huenda ukafungua ukurasa mpya nchini humo.

Chama tawala ANC, kipo katika hatari ya kupoteza wingi wake wa viti bungeni.

Uchaguzi huo unaonekana muhimu zaidi tangu mpigania uhuru na kisha baadae kuwa rais, Nelson Mandela alipoiongoza nchi hiyo kupata demokrasia mwaka wa 1994.

Chama cha African National Congress (ANC), ambacho kimetawala nchi hiyo kwa miaka yote tangu kumalizika kwa enzi ya ubaguzi wa rangi, kipo katika hatari ya kupoteza wingi wake wa viti bungeni kwa mara ya kwanza.

Kwa mujibu wa uchunguzi wa maoni, ANC inatarajiwa kupata chini ya asilimia 50 ya kura, katika hali hiyo itahitajika kuunda serikali ya muungano.

Afrika Kusini inakabiliwa na uchumi unaodhohofika, ukosefu wa ajira na umaskini, kukatika kwa umeme mara kwa mara, na huduma mbovu za usambazaji maji.

Pia nchi hiyo inakabiliwa na hali ya kuporomoka kwa mfumo wa huduma za afya pamoja na viwango vya juu vya uhalifu.

Wanachama kutoka vyama 52 wanashindania viti 400 vya bunge la nchi hiyo.

Serikali mpya za mikoa pia zitachaguliwa. Kati ya watu milioni 40.1 wenye uwezo wa kupiga kura, milioni 27.4 wamesajiliwa kupiga kura.

Bunge jipya litakalochaguliwa lazima kisha liunde serikali na kumchagua rais katika kipindi cha siku 14.

Rais Cyril Ramaphosa, alipiga kura yake katika kituo cha Chiawelo katika kitongoji cha Soweto, akiandamana na mkewe Tshepo Motsepe.

Baada ya kukamilisha upigaji kura, alisema ana imani kuwa Tume Huru ya Uchaguzi (IEC) itasimamia uchaguzi vizuri kwa sababu wana kiwango cha kimataifa na wamejipanga vyema.

„Hii ni siku kuu kwa demokrasia nchini Afrika Kusini. Leo tunapigia kura utulivu na upanuzi wa demokrasia yetu," alisema.

Alisema ana matumaini ya kupata nafasi hiyo na kuendelea kuongoza nchi hiyo.

*DW*

## Hatimaye serikali mpya DRC yatangazwa rasmi

**KINSHASA,** DRC

HATIMAYE serikali mpya itakayoongoza Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imetangazwa ikiongozwa na Waziri Mkuu Judith Suminwa.

Serikali hiyo ilitangazwa jana ikiundwa na mawaziri 54, wakiwemo manaibu waziri mkuu sita, mawaziri tisa wa nchi na mawaziri wanne kama wajumbe wa baraza.

Katika orodha hiyo, mawaziri Jean-Pierre Lihau, Eve Bazaiba, Augustin Kibasa na Patrick Muyaya wakiendelea kushikilia nafasi zao.

Jean-Pierre Bembe amehamishwa kutoka wizara ya Ulinzia na kuwa waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano, Jean Lucien Bussa anaondoka kwenye wizara ya Biashara ya Kigenui na nafasi yake imechukuliwa na Julien Paluku.

Miongoni mwa maingizo mapya katika baraza la mawaziri ni Jacquemin Shabani, Naibu Waziri Mkuu wa mambo ya ndani, Guy Kabongo Mwadiamvita, Ulinzi, Daniel Samba Mokoko, Uchumi na Guylain Nyembo, anakuwa waziri wa mipango na uratibu wa misaada ya maendeleo.

Uchaguzi mkuu wa rais ulifanyika Desemba 20, 2023, Rais Félix Tshisekedi alichaguliwa tena kuongoza nchi hiyo kwa asilimia 72 ya kura zilizopingwa.

Kutangazwa kwa serikali mpya imechukua miezi mitano tangu kuapishwa kwa rais na miezi miwili baada ya kuteuliwa kwa waziri mkuu, jambo lililosababisha imekosolewa vikali na wadau wa kisiasa na kuashiria mgawanyiko ndani ya muungano vyama tawala.

*RFI*

## Stars kujipima kwa Indonesia

**Na Faustine Feliciane**

KIKOSI cha timu ya soka ya taifa ,Taifa Stars' kinatarajia kucheza mchezo wa kimataifa wa kirafiki dhidi ya Indonesia Jumapili ijayo ikiwa ni maandalizi kabla ya kukabiliana na Zambia kwenye mchezo wa kufuzu kombe la Dunia.

Stars itacheza na Indonesia usiku wa saa 6:00 kwa saa za hapa nyumbani, mchezo huo umepangwa kucheza kwenye uwanja wa Madya Gelora Bung Karno Jijini Jakarta.

Kwa mujibu wa Shirikisho la soka Tanzania (TFF), baada ya mchezo huo, Stars watarejea nchini tayari kuelekea Zambia kukabiliana na wenyeji wao katika mchezo huo wa kufuzu fainali za kombe la Dunia, mchezo huo utakaochezwa Juni 11 kwenye uwanja wa Levy Mwanawasa, Jijini Ndola.

Wapinzani wengine wa Taifa Stars Kundi E kufuzu Kombe hilo la Dunia la mwaka 2026, ni Morocco, Niger, Kongo na Eritrea ambayo hata hivyo imejitoa katika mbio za kuwania tiketi ya kufuzu fainali hizo zinazoandaliwa kwa pamoja na nchi za Canada, Mexico na Marekani.

Taifa Stars ilianza vyema kampeni zake baada ya kupata ushindi wa wa bao 1-0 dhidi ya Niger, Novemba 18 mwaka jana kwenye uwanja wa Marrakech nchini Morocco.

Bao hilo pekee la Stars lilifungwa na mshambuliaji Charles M'Mombwa anayecheza soka la kulipwa nchini Australia.



**Msanii wa filamu Tanzania, Steven Mengere (katikati), akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutambua Tasnia ya Filamu na kuwaahidi kuwapeleka nje kwa ajili ya kujifunza masuala mbalimbali ya sanaa. Kushoto ni Mwenyekiti wa Chama cha Waigizaji Tanzania, Chili Mchomo na kulia ni Msanii Johari. PICHA: IMANI NATHANIEL**



# DUBE AMPA FEI TOTO TUZO MCHEZAJI BORA WA MWAKA

## TPBRC KUTOA ELIMU KWA MABONDIA KUJUA HAKI ZAO

**Na Shufaa Lyimo**

KAMATI ya mpito ya Kamisheni ya ngumi za kulipwa Tanzania (TPBRC) inajipanga kutoa elimu kwa mabondia hapa nchni ili waweze kufahamu haki zao.

Akizungumza na Nipashe jana, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Alex Galinoma, alisema wamegundua mabondia wengi hapa nchini wanadhurumiwa haki zao lakini hawajui sehemu ya kukimbilia kwenda kupata msaada.

"Tuna mpango wa kutoa elimu kwa mabondia na tumeshaanza mchakato, kwa kipindi hiki kifupi cha uongozi tulichokaa tumebaini kuwa asilimia kubwa ya mabondia wanashindwa kupata msaada kwa kuwa hawajui sehemu ya kukimbilia, hii inapelekea wengi kudhurumiwa," aliema Galinoma.

Aidha, alisema imefikia hatua bondia anapigana bila pesa yoyote na kudai muandaaji anampa vitisho asiseme kama amepigana bila pesa.

Alisema mbali na kuwapa mafunzo mabondia vile vile elimu hiyo wataitoa kwa waandaaji wa mapambano, ambao wanaandaa mapambano huku mikataba yao ikiwa haijakidhi vigezo vya kuendesha shughuli hizo.

"Baadhi ya waandaaji wamekuwa wakiandaa mapambano huku mikataba yao ikiwa na mapungufu mengi, hii si sawa, wengine hawamalizani kabisa na mabondia, hili hatulilitaki na ndiosababu tunaanza kwanza kutoa elimu kwao," alisema Galinoma. Kamati hiyo iliteuliwa hivi karibuni na Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo Dk Damas Ndumbaro baada ya uongozi uliokuwepo awali kubainika kuwa na mapungufu ikiwemo madaraka mabovu ya uongozi.

Kamati hiyo juzi ilitangaza kutotambua pambano la bondia Hassan Mwakinyo na Patrick Alloteya kutoka Ghana mbalo lilikuwa lifanyike Mei 31 mwaka huu.

**Na Adam Fungamwango**



MSHAMBULIAJI Prince Dube, amesema kiungo mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum ,Feitoto' anastahili kuwa mchezaji bora wa msimu huu kwa kile alichokionyesha msimu wa 2023/2024 uliomalizika juzi.

Dube ambaye alicheza na Feitoto msimu uliopita kabla ya Mzimbabwe huyo kuingia kwenye mgogoro wa kimkataba na timu hiyo, alisema kwa maoni yake anaona akiachana na tuzo ya ufungaji bora ambayo hupatikana kwa aliye na mabao mengi, lakini kwa upande wa tuzo ya ,MVP', anastahili kuipata Feitoto kwa sababu mbalimbali alizozitoa.

„Ukiachana na mabao mengi msimu huu, aina ya uchezaji wake wa kupiga mashuti, aina ya pasi zake anazotoa kwa wachezaji wenzake, nidhamu yake uwanjani ni kubwa, halafu siyo mchezaji mkorofi uwanjani na nje pia amekuwa na nidhamu kubwa kwa wenzake na jamii inayomzunguka, lakini ni ukweli kuwa amechangia sehemu kubwa kwa Azam kumaliza hapa ilipomaliza", alisema Dube.

Mzimbabwe huyo alifafanua kuwa hana maana kuwa wachezaji wengine si wazuri, ila kwa upande wake anaona msimu huu Feitoto anastahili kubeba tuzo ya uchezaji bora wa msimu.

„Nikisema hivyo, simaanishi wachezaji wengine hakuna walichokionyesha au kukitoa, hapana, kwangu mimi Feitoto amefanya makubwa msimu huu, ameonyesha uwezo mkubwa, kwangu mimi Feitoto anastahili tuzo hii ya mchezaji bora wa msimu," alisema Dube.

Aidha, Dube aliendа mbali na kusema kama angetakiwa kuchagua mchezaji bora kwa upande wa magolikipa tuzo yake angeipeleka kwa golikipa wa Yanga, Djigui Diarra.

Dube alisema Diara amefanya kazi kubwa sana ambapo moja sifa yake kubwa uwanjani ni kuanzisha mashambulizi kwa muda unaotakiwa, au kuupoza mchezo pale inapohitajika.

„Diarra anasifa nyingi za ziada, ni zaidi ya golikipa akiwa uwanjani, anastahili ya kupata tuzo ya golikipa bora wa msimu," alisema Dube.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CASEMIRO NA SAUDIA

KLABU kadhaa za ligi kuu ya Saudia (Saudi Pro), ikiwemo Al Nassr, Al Ahli na Al Qasidiya, zinawania kumsajili kiungo wa kati wa timu ya taifa ya Brazil, Casemiro mwenye umri wa miaka 32, kutoka Manchester United msimu huu. ***(Goal)***

### BRUNO ANUKIA WEST HAM

KLABU ya West Ham imefikia makubaliano ya mkataba wa pauni milioni 15 na Flamengo kumnunua mlinzi wa Brazil, Fabricio Bruno mwenye umri wa miaka 28. ***(Guardian)***

### MASON ANAITAKA GETAFE

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Mason Greenwood anataka kurejea katika klabu ya Getafe msimu ujao baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 hivi majuzi kucheza mechi yake ya mwisho kama mchezaji wa mkopo katika klabu hiyo ya La Liga. ***(TEAMtalk)***

### BROWN AWANIWA VILLA

KLABU ya Aston Villa na Crystal Palace zinatazamia kumnunua beki wa Gent, Archie Brown mwenye umri wa miaka 22. ***(Mirror)***

### FELIX KUREJEA BARCA

KLABU ya Barcelona huenda wakamrejesha Nou Camp kwa mara ya pili mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix kutoka Atletico Madrid. ***(Sport)***

### ADARABIOYO AWANIWA

KLABU ya Newcastle United inashinikiza kupata jibu kuhusu uwezekano wa kumnunua beki wa England, Tosin Adarabioyo, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 akitarajiwa kuondoka Fulham msimu huu wa majira ya joto mkataba wake utakapomalizika. ***(Talksport)***

### DEN BERG ANYATIWA

LIVERPOOL imeweka thamani ya pauni milioni 20 kwa mlinzi wa Uholanzi, Sepp van den Berg mwenye miaka 22, ambaye ananyatiwa na klabu za Brentford, Southampton na Wolfsburg baada ya kung'aa akiwa na Mainz kwa mkopo. ***(Athletic)***

### KVARATSKHELIA HAUZWI

KLABU ya Napoli haina nia ya kumuuza winga wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia mwenye umri wa miaka 23 kwa PSG, huku Antonio Conte akitarajiwa kuwa kocha wao mpya. ***(Corriere dello Sport)***

### RODRYGO HATIHATI

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid na Brazil, Rodrygo mwenye miaka 23, ametilia shaka mustakabali wake katika klabu hiyo, na hivyo kuongeza uwezekano wa kuhamia Liverpool. ***(Mundo Deportivo)***

### OLMO AWA LULU ULAYA

KINYANG'ANYIRO cha kumsaka mshambuliaji wa RB Leipzig na Hispania, Dani Olmo kimeshika kasi, huku Barcelona, Manchester United, Manchester City, Liverpool na Bayern Munich zikimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. ***(Mundo Deportivo)***

### CLARKE KUTUA S' AMPTON

KLABU ya Southampton inawania saini ya winga wa Sunderland, Jack Clarke mwenye umri wa miaka 23. ***(Telegraph)***




# LIVERPOOL YATAKA SAINI YA ÉDERSON

●●●Huo unaweza ukawa usajili wa kwanza wa kocha mpya wa timu hiyo ambaye...

**LIVERPOOL,** ENGLAND


TETESI za usajili zinasema Liverpool inajiandaa kuanza mchakato wa kumsajili kiungo mkabaji Éderson José dos Santos Lourenço da Silva, 'Éderson' wa Atalanta katika kile kinachoweza kuwa usajili wa kwanza wa kocha mpya wa The Red, Arne Slot.

Éderson alikuwa na msimu bora Atalanta, akifunga mabao 6 na kutoa pasi 1 ya bao katika michezo 35.

Amecheza mechi 52 katika mashindano yote ya kikosi bingwa cha Kombe la Ligi ya Europa cha kocha Gian Piero Gasperini akionesha kiwango kilichomfanya kuitwa timu ya taifa ya Brazil kwa ajili ya michuano ijayo ya Copa America.

Éderson ana miaka mitatu katika mkataba wake na Atalanta lakini inaonekana kama ofa za usajili toka Ligi Kuu Engkand zinaibuka tena baada ya kuhusishwa na Newcastle United na Tottenham Hotspur Januari, 2024.

# GREENWOOD KWENYE RADA ZA DORTMUND




**DORTMUND,** UJERUMANI

KLABU ya Borussia Dortmund haijaondoa uwezekano wa kumnunua fowadi wa Manchester United, Mason Greenwood na watapiga simu baada ya mechi ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid Jumamosi.

Greenwood mwenye umri wa miaka 22, anatarajiwa kurejea Old Trafford msimu huu wa joto baada ya kukaa kwa mkopo katika klabu ya LaLiga ya Getafe, ambapo alifunga mabao 8 katika mechi 33 za ligi na kutajwa kuwa mchezaji wao bora wa msimu.

Juventus na Atlético Madrid zimehusishwa kutaka kumnunua pia na Dortmund ambayo ilimchukua winga Jadon Sancho kwa mkopo kutoka United Januari, wameonekana kuwa huenda wakatua kwa Greenwood, ambaye amebakiza mwaka mmoja kumalizia mkataba wake na United. Ripoti kutoka Ujerumani zimedokeza kwamba Dortmund iko tayari kumchukua Greenwood kwa mkopo na, akizungumza na vyombo vya habari vya klabu hiyo, Mkurugenzi wa michezo, Sebastian Kehl alisema mipango yote imesitishwa hadi baada ya pambano la Jumamosi la Wembley dhidi ya Madrid.

"Sitaki kuzungumza kuhusu uvumi wowote kwa sasa kwa sababu haina maana," Kehl alisema. "Wacha tucheze fainali hiyo Jumamosi.

"Ni kweli tuna mipango yetu ya msimu ujao na bila shaka tunajadili matukio mengi, lakini hakuna kitu kwa leo. Hebu tuzingatie, tutarajie mechi hiyo Jumamosi kisha tutaona jinsi tunavyosonga mbele."

Alipoulizwa kama Greenwood ni mchezaji ambaye Dortmund inamvutia, Kehl alisema, "Sitaki kuzungumzia hilo sasa."

## Eto'o, kocha mpya Cameroon vita kali

**YAOUNDE,** CAMEROON

SOKA la Cameroon lilitumbukia katika mgogoro mkubwa juzi wakati mkutano kati ya rais wa Shirikisho la soka, Samuel Eto'o na kocha mpya wa nchi hiyo Mbelgiji Marc Brys ulipogeuka kuwa wa vurugu.

Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Eto'o kukutana na Brys, ambaye aliteuliwa na Wizara ya Michezo ya nchi hiyo mapema Aprili bila maoni yoyote kutoka kwa Shirikisho hilo, na kuanzisha mzozo kati ya wawili hao.

Brys alikuwa amealikwa kwa "kikao cha kazi" na Eto'o wakati Cameroon inapojiandaa kwa mechi za kufuzu Kombe la Dunia mwezi ujao, lakini baadhi ya wasaidizi wake ambao pia waliteuliwa na Wizara ya michezo, walikataliwa kuingia katika jengo la shirikisho la FECAFOOT mjini Yaounde.

Video inayosambaa kwenye tovuti kadhaa za mitandao ya kijamii, iliyorekodiwa na wanahabari, inaonesha Eto'o akimkaribisha Brys lakini mabadilishano yao yalibadilika haraka na kuwa vurugu.

Kwanza Eto'o kwa hasira alimfukuza Ofisa wa wizara ambaye alitaka kuhudhuria mkutano huo, na kisha akawa na mabishano makali na Brys, ambaye aliondoka mara moja.

Taarifa inatarajiwa baadaye kutoka kwa FECAFOOT, ambao walikuwa wameelezea nia ya kufanya kazi na Mbelgiji huyo licha ya awali kukashifu uteuzi wake kama uamuzi wa upande mmoja na waziri wa michezo, Narcisse Mouelle Kombito.

Kwa kawaida, Shirikisho la soka lingeteua na kuwalipa makocha wake lakini katika baadhi ya nchi za Afrika jambo hili hufanywa na serikali hasa pale mashirikisho yanapokuwa na uhaba wa fedha.

Mwanasoka Bora wa zamani wa Afrika, Eto'o, amejaribu kudai uhuru lakini pia amelazimika kukanyaga kwa uangalifu katika nchi ambayo masuala yanayohusu timu ya soka yanapewa kipaumbele na serikali.

Rais wa muda mrefu wa Cameroon, Paul Biya mara nyingi amekuwa akiweka uzito katika masuala ya timu, alitaka Roger Milla aliyekuwa na umri wa miaka 38 ajumuishwe kwenye kikosi cha Kombe la Dunia la 1990.

Mshambuliaji huyo mkongwe alifunga mabao muhimu huku Cameroon ikiwa nchi ya kwanza ya Afrika kutinga robo fainali.

Cameroon imefuzu kwa michuano nane ya Kombe la Dunia, zaidi ya nchi nyingine Afrika.



## Rodrygo aibua hofu Real Madrid

**MADRID,** HISPANIA

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Rodrygo ameibua hasira za mashabiki kadhaa baada ya taarifa za kutatanisha kuhusu mustakabali wake katika klabu hiyo siku chache kabla ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Huku ujio wa Kylian Mbappe Santiago Bernabeu ukitarajiwa kutangazwa hivi karibuni, jukumu la Rodrygo katika kikosi cha Carlo Ancelotti linaonekana kuwa hatarini na amekuwa akihusishwa mara kwa mara na kuhamia Ligi Kuu ya England.

Akizungumza na DAZN katika maandalizi ya fainali ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Borussia Dortmund Juni 1, Rodrygo alisisitiza nia yake ya kusalia Madrid lakini alikataa kuondoa uwezekano wa kuondoka.

Alipoulizwa kama anataka kubaki na Madrid milele, Rodrygo alijibu: "Ndiyo. Naam... lolote linaweza kutokea. Nina mkataba hapa, lakini sijui.

"Miaka ambayo nimekuwa hapa imekuwa furaha kwangu."

Ilipoelezwa kuwa maoni yake yanaweza kuwatoa jasho Madrid, Rodrygo kwa mara nyingine alikataa kutoa taarifa za uhakika.

"Siku zote nimesema nataka kuwa katika klabu hii, lakini tuone," alijibu. Kujibu maoni ya Rodrygo, Mundo Deportivo limesema kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 bado analengwa na Ligi Kuu England, ambapo Liverpool wanaongoza katika mbio za kuwania saini yake.

Ripoti hiyo inaongeza kuwa wawakilishi wa Rodrygo wamejaribu haraka kupunguza uvumi huo kwa kusisitiza kuwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil hataki kuondoka Madrid, huku viongozi wa klabu hiyo pia wakitaka kumshikilia Rodrygo licha ya kuwasili kwa Mbappe.

Mkataba wa Rodrygo na Madrid bado una miaka minne kukamilika baada ya kusaini nyongeza Novemba 2023.

HABARI MICHEZO

# AZIZ KI, FEITOTO WAPONGEZANA

**Na Faustine Feliciane**

LICHA ya kuibuka mfungaji bora wa Ligi Kuu msimu uliomalizika juzi, kiungo wa Yanga amemsifu na kumpongeza nyota wa Azam FC, Feisal Salum 'Feitoto' kwa upinzani mkali aliounyesha kwenye kuwania tuzo hiyo.

Aziz Ki alisema, Fei toto ameonyesha uwezo mkubwa msimu huu akiichezea Azam baada ya kuondoka Yanga na alikuwa mpinzani wa kweli kwenye mbio hizo za kuwania tuzo hiyo ya mfungaji bora msimu huu.

Alisema ameshukuru kumaliza ligi akiwa mfungaji bora na anaamini mabao aliyoyafunga yamechangia kwa timu yake kuchukua ubingwa msimu huu.

Aziz Ki amemaliza ligi akiwa na mabao 21 akimzidi Feitoto mabao mawili baada ya kuchuana kwa muda mrefu lakini mechi za mwisho juzi ziliamua nani wa kutwaa tuzo hiyo.

„Nafurahi nimeisaidia timu yangu kuchukua ubingwa na mimi kumaliza na mabao mengi, nawashukuru wachezaji wenzangu kwa ushirikiano wao, lakini siwezi kuacha kumsifia Feitoto, tulichuana kwa muda mrefu, ni mchezaji mzuri na ameonyesha uwezo mkubwa sana akiwa na timu yake, binafsi namkubali sana," alisema Feitoto.

Alisema anampongeza sana Feitoto na ameonysha yeye ni mchezaji mkubwa na mwenye kipaji Tanzania.

Kwa upande wake, Feitoto alimpongeza mchezaji mwenzake huyo wa zamani ndani ya Yanga kwa kumaliza Ligi akiwa mfungaji bora.

„Hongera sana kwake kwa kumaliza akiwa na mabao mengi, namfahamu ni mchezaji mzuri na kwa kile alichokionyesha anastahili pongezi," alisema Feitoto.

Alisema kama mchezaji anafuraha kuona timu yake imefuzu kucheza michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kumaliza katika nafasi ya pili nyuma ya mabingwa, Yanga.

„Lengo la kwanza ilikuwa kuisaidia timu kufuzu kwa michuano Ligi ya Mabingwa Afrika, nashukuru Mungu tumefanikiwa, kukosa tuzo ya kiatu kwangu sio kitu kama tungekosa tiketi ya kushiriki michuano hiyo," alisema Feitoto.



Mwanafunzi wa Shule ya Msingi Gerezani, Hamis Ali (chini), akizuia mpira huku akizongwa na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Jamhuri, walipokuwa wakicheza mechi ya kirafiki katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Tuzo wachezaji bora Ligi Kuu kutolewa msimu ujao

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF) limetangaza tuzo za wanamichezo bora wa Ligi Kuu zinatarajiwa kutolewa kwenye mechi za Ngao ya Jamii ya kufungua pazia jipya la ligi hiyo msimu wa 2024/2025.

Mabadiliko hayo yamefanyika ili kulifanya tukio hilo kuwa kubwa, bora zaidi na kukidhi malengo na mahitaji yake.

Taarifa iliyotolewa jana na Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Cliford Ndimbo, alisema hafla za kuwatunza wanamichezo bora wa msimu ambazo zilikuwa zinatolewa wiki chache baada ya ligi kumalizika, sasa zitatolewa kuelekea kwenye kufungua msimu wa Ligi Kuu 2024/25, wakati wa mechi hizo za Ngao ya Jamii, ambazo huwa ni maalum kwa ajili ya kufungua msimu.

„Lengo la mabadiliko ya hafla hizo za kuwatunza wachezaji bora wa msimu ni kufanya maboresho ya kulifanya tukio kuwa bora zaidi kukidhi malengo na mahitaji, lakini pia kulipa thamani zaidi," alisema Ndimbo kwenye taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema mabadiliko hayo pia yatasaidia wahusika wote wa tuzo hizo hususani wachezaji wanakuwapo kwenye hafla hiyo.

„Mara nyingi ligi ikimalizika wachezaji wengi wanaondoka, wa nje ya nchi wanakwenda kwao, na hata wa hapa wanarudi majumbani kwao mikoani kupumzika, kwa hiyo wanajikuta wanakosekana na kuzifanya kudorora na zikose mvuto, sasa tumeona tufanye kipindi cha michezo ya Ngao ya Jamii ambapo wachezaji wote wanakuwepo. Kama msimu uliopita ndivyo tatukavyofanya kwa kushirikisha timu nne kwenye michezo hii ya Ngao ya Jamii," ilisema taarifa hiyo. Wachezaji ambao tayari wana uhakika wa tuzo baada ya msimu kumalizika juzi, ni Stephane Aziz Ki ambaye ni mfungaji bora baada ya kumaliza ligi akiwa na mabao 21, kipa bora, Ley Matampi, ambaye amemaliza akiwa na 'clean shit' nyingi, amekaa langoni kwenye mechi 15 mfululizo bila kuruhusu bao.



## Yanga yavunja rekodi zake msimu uliopita

INATOKA UK. 24

huu imeshika nafasi ya tatu, ikiambulia kucheza Kombe la Shirikisho msimu ujao, imeshindwa angalau kufikia rekodi yake iliyoweka kwenye Ligi Kuu msimu uliopita, achilia mbali kuvunja.

Imemaliza Ligi ikiwa na pointi 69, pointi nne nyuma ya zile ilizopata msimu uliopita ambapo ilivuna pointi 73, huku pia msimu huu ikiruhusu mabao 25, manane zaidi ya msimu uliopita, iliporuhusu mabao 17 tu.

Timu hiyo msimu huu imepata ushindi mara 21, ikishindwa kuifikia rekodi ya msimu uliopita iliposhinda mara 22, pia msimu uliopita ilipoteza mchezo mmoja tu, msimu huu imepoteza mechi tatu.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alikiri kuwa haukuwa msimu mzuri kwa sababu hawakutimiza malengo yao.

„Msimu huu hatukutimiza malengo yetu kwa asilimia 90, lakini huo ndiyo ushindani, tuna nafasi kubwa ya sisi wenyewe kujiangalia wapi tumekosea, ukiangalia sehemu kubwa ya makosa tuliyoyafanya ni yetu sisi wenyewe, inabidi sasa kukaa na kuangalia wapi pa kurekebisha ili msimu ujao turejee tukiwa bora zaidi," alisema Ahmed.

## Nyota Simba SC watoa ya moyoni

INATOKA UK. 24

tatizo na watakaa kurekebisha kwa ajili ya msimu ujao.

„Tunashukuru tumemaliza ligi salama, matokeo hayajawa mazuri kwetu na kwa mashabiki wetu, lakini ndio mpira ulivyo, viongozi wetu watakuwa wameona wapi kwenye tatizo, watakaa chini na kuona nini cha kufanya ili kuirejesha timu kwenye nafasi yake," alisema Ntibazonkiza.

Alisema anaamini msimu ujao Simba itarejea kwa nguvu na kurudi kwenye ubora wake.

Kutokana na kumaliza kwenye nafasi ya tatu msimu huu, Simba itaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho pamoja na Coastal Union.

Michezo
Alhamisi Mei 30, 2024
Nipashe

**Liverpool yataka saini ya Éderson**



UKURASA 21



Wachezaji wa Yanga wakishangilia ushindi kwenye moja ya mechi zao katika msimu uliomalizika juzi. **PICHA: MAKTABA**

# Yanga yavunja rekodi zake msimu uliopita

●●● Mtani wao ashindwa hata kuzifikia rekodi zake, akimaliza ligi nafasi ya tatu...

**Na Adam Fungamwango**

HUKU ikitwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa misimu mitatu mfululizo, Yanga imefanikiwa kuvunja rekodi zake za msimu uliopita, huku watani zao wa jadi Simba wakishindwa kufanya hivyo, ikiishia nafasi ya tatu kwenye msimamo.

Kwa mujibu wa dawati letu la takwimu, Yanga ambayo imekata tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao, imemaliza mechi zake 30 msimu huu ikijikusanyia pointi 80, na kuvunja rekodi ya msimu uliopita ilipomaliza ikiwa na pointi 78, hivyo msimu huu imezidi pointi mbili zaidi.

Msimu huu, Yanga imemaliza ligi ikishinda michezo 26, hivyo kuvunja rekodi ya msimu uliopita iliposhinda michezo 25, ambapo imezidi mchezo mmoja mbele.

**Mabingwa hao msimu huu wameongeza idadi ya mabao 10 zaidi ya msimu uliopita, kwani wamepachika mabao 71, wakivunja rekodi ya msimu uliopita, walipomaliza na mabao yao 61, huku pia ikiruhusu idadi ndogo ya mabao ambayo ni 14 tu, wakati msimu uliopita iliruhusu mabao 18, hivyo kuwa pungufu ya mabao manne msimu huu.**

Rekodi nyingine ya kujivunia kwa Yanga msimu huu ni kushinda mechi zake zote 15 nyumbani, huku ikipata sare mechi tatu ugenini na kupoteza mechi mbili.

Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, akizungumza muda mfupi baada ya kumalizika kwa ligi hiyo juzi, alisema wamekuwa na msimu bora, wakiweka na kuvunja rekodi nyingi, akiisifu timu yake kuwa ilikuwa timu ya kutisha msimu huu.

„Tumetengeneza rekodi nyingi na tumevunja rekodi nyingi msimu huu, tumepata pointi nyingi sana, tumefunga mabao ya kutosha na tumeruhusu mabao machache, sitaki kuzungumzia 'hat-trick' hapa wala 'asisti', rekodi hizo za klabu zinatosha kuonyesha tulikuwa timu bora," alisema Gamondi.

Kwa upande wa Simba ambayo msimu

INAENDELEA UK. 23

# Nyota Simba watoa ya moyoni

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kushuhudia Simba ikimaliza nafasi ya tatu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, baadhi ya nyota wa timu hiyo wamefunguka nini kifanyike kwa ajili ya kuirejesha timu hiyo kwenye ubora wake.

Simba imemaliza ligi kwenye nafasi ya tatu nyuma ya Azam na Yanga na sasa itashiriki michuano ya Shirikisho Afrika hiyo ikiwa ni mara ya kwanza baada ya misimu sita mfululizo ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza juzi, beki wa kati wa timu hiyo, Che Malone, alisema matokeo mabaya waliyoyapata msimu huu yametokana na sababu mbalimbali ikiwamo ya uongozi, usajili na maandalizi ya timu kabla ya kuanza kwa ligi.

Alisema kuwa lazima waweke sawa baadhi ya mambo ili kurejea kwenye ubora wao msimu ujao.

„Hili si suala la mtu mmoja mmoja, kila mtu anahusika kuanzia uongozi mpaka wachezaji, tunatakiwa kuweka mambo sawa kuanzia kwenye uongozi, aina ya usajili na hata maandalizi ya timu kabla ya kuanza ligi," alisema Malone.

Alisema lazima uongozi ukae imara na kufanya usajili wenye tija pamoja na kuchagua eneo sahihi la kufanya maandalizi kuelekea kwenye msimu mpya.

„Hatuwezi kumlaumu mtu mmoja, lazima wote tujitathmini na kuweka mikakati imara ya kuirejesha timu kwenye ubora wake, Simba ni timu kubwa," alisema nyota huyo raia wa Cameroon.

Kwa upande wake, mshambuliaji wa timu hiyo raia wa Burundi Saido Ntibazonkiza, alisema anaamini viongozi wameona wapi kwenye

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042